

# Utafiti kuhusu Upatikanaji wa Elimu ya Awali Jumuishi kwa Watoto wenye Ulemavu

Juni

2020

hakielimu

# Utafiti kuhusu Upatikanaji wa Elimu ya Awali Jumuishi kwa Watoto wenye Ulemavu

Juni

2020

# Shukrani

HakiElimu inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, (MoEST), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Ofisi ya Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), maafisa mbalimbali ngazi ya mkoa na wilaya, wakuu wa shule, walimu, wazazi na wanafunzi wote walioshirki utafiti wetu kutoka wilaya zote tulizozifikia kwenye utafiti huu.

Utayari na msaada wenu umesaidia sana kuifanya ripoti hii isheheni taarifa za kina. Pia HakiElimu inatambua mchango wa Dk Richard Shukia (PhD) kutoka Idara ya Saikolojia ya Elimu, Shule kuu ya Elimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambaye kwa niaba ya HakiElimu alionoza timu ya utafiti, kwa msaada wa kiufundi kutoka kwa Dk John Kalage, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu; Mwemezi Makumba, Rose Kalage, Florige Lyelu (Idara ya Utafiti, Ubunifu na Uchambuzi wa Sera-HakiElimu). Uhariri ulifanywa na Robert Mihayo na Dr. Ellen Otaru (Kitengo chaUhariri na uhakiki wa ubora). Utafiti huu umefanyika kwa kushirikiana na Mtandao wa Elimu kamili kwa Wote/All in, All Learning (AIAL).

Mtandao wa AIAL, unafadhiliwa na Shirika la misaada la Kimataifa la Uingereza UKAid na shirika la Comic Relief, uliundwa mwaka 2017 kwa lengo la kukuza ujifunzaji na ushirikiano kati ya mashirika mbalimbali yanayofanya kazi katika sekta ya elimu au kuhamasisha ujumuishaji nchini Tanzania. Wanachama wa mtandao huu ni pamoja na: Able Child Africa, Action on Disability and Development, ADP Mbozi, Aga Khan Foundation Tanzania, Amani Girls Home (AGH), Assist People with Disabilities Mwanza (APDM), Child Support Tanzania, Education International, Elimu Community Light (ECOLI), Firelight Foundation, HakiElimu, Leonard Cheshire and Tanzania Cheshire Foundation, Madrasa Early Childhood Programme, Miyuji Cheshire Home, Mwanza Women Development Organisation (MDWO), Organisation For Community Development (OCODE), Sawa Wanawke Tanzania (SAWA), Save the Children Tanzania, Sazani Associates, Seeds for Future Organisation (SEFFO), SHIVYAWATA, Tanzania Home Economics Association (TAHEA) Mwanza, Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Tanzania Maendeleo Kwanza (TMK), Umoja for Sustainable Society Development (USSD) na Women Against AIDS in Kilimanjaro (KIWAKKUKI).

**HakiElimu @ 2020**

**ISBN 978-9987-18-077-6**

Sehemu yoyote ya chapisho hili inaweza kunukuliwa kwa madhumuni ya kielimu yasiyo ya kibiashara, ilimradi tu chanzo kitajwe na angalau nakala moja ipelekwe HakiElimu

# Yaliyomo


Shkrani i

Muhtasari wa Utafiti iv

1 Mukatadha wa Usuli wa Utafiti 1
1.1 Malengo 3
1.2 Dhana Muhimu na Fasili zake 3
1.3. Nadharia ya Wazo: 4

2 Mbinu za Utafiti 5
2.1. Maeneo ya Utafiti na Washiriki 5
2.2. Mbinu za Kukusanya Takwimu na Taarifa 6
2.3. Usimamizi, Uchakataji na Uchambuzi wa Data 8
2.4. Hatua za Kudhibiti Ubora 8
2.5. Maadili ya Utafiti na Usalama 9

3 Matokeo ya Utafiti 10
3.1 Mazingira ya Kisera na kisheria 10
3.2 Upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto wenye ulemavu 14
3.3 Mwenendo wa Uandikishaji watoto wenye ulemavu ki-mkoa, 2016-2020 16
3.4. Kiwango cha kuhitimu & kuvuka darasa cha wanafunzi wenye ulemavu (awali kwenda drs I) 18
3.5. Sababu zinazozuia watoto wenye ulemavu kupata elimu 19
3.6. Utayari wa shule na madarasa kutoa elimu jumuishi ya awali 21
3.7. Mpangilio wa darasa na hali ya hewa 23
3.8 Ufundishaji na Ujifunzaji 25
3.9. Mambo mengine yanayozuia elimu jumuishi 26
3.10. Utofauti wa miundombinu ya shule kwa makundi ya shule 28
3.11 Utendaji wenye mafanikio 28

4 Hitimisho na Mapendekezo 31
4.1. Hitimisho 31
4.2. Mapendekezo 32

5 Marejeo 33

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| AIAL | All In All Learning/Ujifunzaji Kamili kwa Wote |
| BEST | Basic Education Statistics Tanzania/ Takwimu za ElimuMsingi Tanzania |
| CCI's | Cross-Cutting Issues/Masuala Mtambuka |
| CRPD | Convention on Rights of People with Disabilities/ Mkataba wa Haki za Watu wenye ulemavu |
| CWDs | Children with Disabilities/Watoto wenye Ulemavu |
| DAO | District Academic Officers/Maafisa Taaluma Wilaya |
| DEO | District Education Officer/Afisa Elimu Wilaya |
| ECE | Early Childhood Education/Elimu ya makuzi na malezi ya awali |
| FGD | Focus Group Discussion/Vikundi Mjadala |
| GRE | Gross Enrolment Rates/Uandikishaji wa Jumla |
| LGA's | Local Government Authority/Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| MoEST | Ministry of Education, Science and Technology/Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| NER | Uandikishaji Halisi |
| PO-RALG | President's Office, Regional Administration and Local Government Tanzania/Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Tanzania(TAMISEMI) |
| PPE | Elimu ya Awali |
| QA | Quality Assurers/Wathibiti Ubora wa Shule |
| RAO | Regional Academic Officer/Afisa Taaluma Mkoa |
| REO | Regional Education Officer/Afisa Elimu Mkoa |
| SDG | Sustainable Development Goals/Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| SWO | Social Welfare Officers/Maafisa Ustawi wa jamii |
| TAMH | Tanzania Association for Mentally Handicapped/Chama cha Watu wenye ulemavu wa akili |
| TIE | Tanzania Institute of Education/ Taasisi ya Elimu Tanzania |
| UN | United Nations/Umoja wa Mataifa |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation/Shirika la Umoja wa Mataifa la sayansi na Utamaduni |
| URT | United Republic of Tanzania/Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| VEO/MEO | Village Executive Officer/Afisa Mtendaji wa Kijiji |
| WEC | Ward Executive Coordinators/Waratibu Elimu Kata |
| WEO | Ward Education Officer/Afisa Elimu Kata |

## Muhtasari wa Utafiti

Elimu-jumuishi ina lengo la kuondoa vizuizi ndani ya mifumo ya elimu ambavyo huwatenga watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu pamoja na wale wenye ulemavu. Elimu jumuishi inazitaka shule, walimu na madarasa kubadilika ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu. Tanzania, imeridhia na inafuata sheria na mikataba ya kimataifa ili kuhakikisha elimu-jumuishi inatekelezwa nchini. Ili kufanikisha hili, Sera ya Taifa ya Huduma kwa watu wenye Ulemavu ya 2004 inasema wazi kuwa ni muhimu kufanya utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu, ili wapatiwe huduma stahiki mapema. Sambamba na sera hii, Taasisi ya Elimu Tanzania imeandaa Mitaala ya Elimu ya Awali (ECE) ambayo inahitaji walimu kufanya utambuzi wa mapema wa watoto wenye mahitaji maalum na kutoa huduma stahiki. Ingawa, elimu ya awali inahimiza ujumuishaji, haijulikani sana na kuna taarifa chache kuhusu kiwango ambacho kanuni jumuishi zinatafsiriwa kwa vitendo hapa nchini.

HakiElimu iliratibu utafiti kwa niaba ya "Mtandao wa Ujifunzaji kamili kwa Wote" (Mtandao wa AIAL) kuchunguza upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto wenye ulemavu. Utafiti ulilenga kuangalia hali halisi ya mazingira na muktadha kwa ujifunzaji pamoja mifumo ya kitaasisi ambavyo vinawazuia watoto wenye ulemavu kujiunga na shule na kushiriki kikamilifu kwenye elimu jumuishi ya awali, na kisha kupendekeza njia za kuboresha fursa za elimu kwa watoto wenye ulemavu. Utafiti huu uliongozwa na malengo mahususi yafuatayo: kuchunguza jinsi sera, miundo na mazingira yaliyopo vinavyosaidia kuwajumuisha watoto wenye ulemavu kwenye mazingira ya utoaji elimu ya awali; kujua idadi ya watoto wenye ulemavu walioandikishwa shule za awali na kuona kama wanajifunza katika mazingira jumuishi; kujua uwiano wa idadi ya watoto wenye ulemavu wanaovuka elimu ya awali na kuendelea elimu ya msingi, na kubainisha vikwazo vya kimazingira na taasisi vinavyowazuia watoto wenye ulemavu kujiunga na shule na kushiriki kikamilifu kwenye elimu ya awali jumuishi.

Utafiti ulitumia mbinu mbalimbali kukusanya takwimu za kiubora na za kiidadi. Mbinu hizi ni pamoja na; uchambuzi wa maudhui ya nyaraka rejea husika, kuwahoji watoa habari muhimu, mahojiano ya kina, majadiliano ya vikundi, uchunguzi darasani na mahojiano ya baada ya uchunguzi. Utafiti ulifanyika katika mikoa kumi ambayo ni; Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Tabora, Shinyanga, Kagera, Mtwara, Njombe, Kilimanjaro na Tanga. Jumla ya wilaya 20 (2 kila mkoa) zilichaguliwa kushiriki kwenye utafiti huo. Mtafiti kiongozi, kwa kushirikiana na maafisa wa elimu mkoa, alibainisha wilaya mbili, yenye utekelezaji 'mkubwa' na yenye utekelezaji 'hafifu' wa elimu jumuishi katika mikoa yao. Wilaya zilichaguliwa kinasibu.

Jumla ya washiriki, 1,238 walihusika katika kujibu maswali yaliyoongoza utafiti huu. Washiriki hawa ni pamoja na maafisa kutoka Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Taasisi za Serikali zenye wajibu wa kushughulikia elimu ya awali na elimu-jumuishi. Aidha, utafiti huo ulijumuisha maafisa elimu kutoka ngazi za mkoa, wilaya, na kata. Katika ngazi ya shule, utafiti uliwahusisha wakuu wa shule, walimu wa awali na wazazi wa watoto walio na wasio na ulemavu.

Matokeo ya uchambuzi wa nyaraka za sera yanaonesha kuwa Tanzania ina mfumo mzuri wa kisheria unaohakikisha haki za watu wenye ulemavu zinazingatiwa katika muktadha na mazingira mbalimbali. Kanuni ya haki sawa ya kupata elimu imeoneshwa katika sera, miongozo na sheria mbalimbali. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa mtaala wa elimu ya awali na silabasi pamoja na miongozo ya kimtaala zinatambua kanuni ya elimu-jumuishi. Kwa mfano; watoto wenye ulemavu wanawakilishwa kwa haki na kuthaminiwa kwenye vitabu vya kiada vya elimu ya awali.

Aidha, utafiti unaonesha kuwa hali ya uandikishaji elimu ya awali inabadilika. Hii inaendana na uandikishaji ngazi ya taifa. Pengo la kijinsia ni dogo sana. Watoto wenye umri wa miaka 5 wameandikishwa kwa idadi kubwa zaidi ikilinganishwa na watoto wenye umri mwingine. Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu katika ngazi ya kitaifa umegawanywa kwa makundi ya aina ya ulemavu na jinsia. Takwimu zinaonesha kuwa uandikishaji wa watoto wenye ulemavu wa viungo na afya ya akili ulikuwa juu kwa miaka yote ikilinganishwa na aina zingine za ulemavu. Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu wa kuona umekuwa uandikishaji mdogo zaidi wa wanafunzi wenye ulemavu kwa miaka yote. Hata hivyo, karibu shule zote, kata, wilaya na mkoa zilizotembelewa hazina takwimu kamili au zilizojumuishwa za watoto wenye ulemavu kama vile takwimu watoto wenye ulemavu na umri wao.

Utafiti unabainisha mambo kadhaa ambayo yanazuia upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto wenye ulemavu. Sababu hizi zinaanzia ngazi ya familia, shule na hadi kwenye jamii. Kuna unyanyapaa dhidi ya watoto wenye ulemavu na kusita kuwaandikisha shuleni. Wazazi wengine waliripotiwa kuficha watoto wao nyumbani. Umbali wa kwenda na kurudi shuleni, ukosefu wa vifaa stahiki vya kujifunzia-kufundishia, ukosefu wa fedha maalum kwa ajili ya watoto wenye ulemavu pamoja na uhaba wa wafanyakazi wenye mafunzo ya elimu maalum ni miongoni mwa sababu zilizobainika kuzuia ushiriki wa watoto wenye ulemavu kwenye mazingira jumuishi.

Utafiti huu unasema kuwa serikali ya Tanzania kupitia sheria na sera zake imedhamiria kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu katika mazingira jumuishi. Watoto wenye ulemavu wenye umri wa kusoma shule ya awali wana fursa ndogo ya kujiunga na shule kutokana na vikwazo vilivyotajwa. Kwenye mazingira ambapo wanapata fursa ya kujiunga na shule, ushiriki wao kwenye mchakato wa kufundishwa na kujifunza ni mdogo. Walimu wengi wana uwezo mdogo wa kusaidia watoto wenye ulemavu. Hii inaweza kuhusishwa na kutopata mafunzo ya elimu maalum. Hivyo, kuna tofauti kubwa kati ya nia ya sera na utekelezaji halisi shuleni. Matokeo ya utafiti wa sasa yanasaidia matokeo ya tafiti mbalimbali za huko nyuma juu ya utoaji wa elimu jumuishi. Utafiti huo unazidi kusema kuwa licha ya juhudi za kutetea na kupigania kuwa na shule jumuishi, shule mchanganyiko na shule maalum bado ni mbinu zinazotumika kuwaelimisha watoto wenye ulemavu. Kwa wingi wa changamoto zinazoikabili shule jumuishi, mbinu ya kutumia shule mchanganyiko ni nzuri zaidi angalau kwa miaka michache ijayo wakati tunafanya jitihada za kuboresha shule jumuishi.

**Mapendekezo**

- Kuboresha uhamasishaji wa jamii unaoendelea kukuza uelewa juu ya hitaji la kuelimisha watoto wenye ulemavu
- Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuhimiza utendaji mzuri unaozingatia ujumuishaji na shughulikia vikwazo vinavyokwamisha juhudi zao zinazoendelea za kukidhi mahitaji ya kielimu ya watoto wenye ulemavu wa elimu ya awali.
- Kuandaa fomu rahisi ya kuwasaidia na kuwaongoza wadau wote wakiwemo walimu wa shule/madarasa ya awali kuwatambua watoto wenye uoni hafifu, ulemavu wa kusikia na changamoto ndogo ya afya aya akili wakati wa kujiunga na shule ya awali.
- Kuandaa miongozo na vigezo vya viwango vya chini vinavyotakiwa kuwepo madarasa ya awali ili viwasaidie na kuwaongoza waalimu juu ya jinsi ya kuyafanya madarasa yao yawe jumuishi zaidi
- Kwa kushirikiana na wadau wengine, serikali inapaswa kuanzisha vituo shikizi ambavyo vitatoa fursa kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali kwenye shule zilizo karibu ndani ya jamii zao.
- Kuongeza bajeti na matumizi ya fedha kugharamia na kusaidia elimu ya awali jumuishi. Njia mojawapo inaweza kuwa kuharakisha utekelezaji wa rasimu ya fomula ya ruzuku ya wanafunzi, ambayo pia inalenga watoto wenye mahitaji maalum shuleni. Utumiaji wa fomula hii unaweza kuhimiza utendaji jumuishi shuleni.
- Kuboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu zinazohusu watoto wenye ulemavu, na zipange takwimu hizo kwa kuzingatia umri, aina ya ulemavu, na jinsia katika ngazi zote.
- Kulimisha watoto wenye ulemavu katika shule maalum au shule mchanganyiko ambako kuna kitengo maalum na walimu maalum wenye ujuzi wa kusaidia watoto wenye ulemavu kujifunza kwa mafanikio.
- Kupitia upya mtaala na silabasi ya elimu ya awali ili kuboresha vifungu vya mitaala vinavyohusiana na viashiria vya utendaji kwa watoto wenye ulemavu wa kusikia na kuona.
- Taasisi ya Elimu Tanzania ifanyie maboresho vitabu vya elimu ya awali na vitabu vya hadithi ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu wa kuona.

# 1. Muktadha wa Utafiti

Kujenga mazingira jumuishi ya kujifunzia ni kipaumbele cha Dunia na kinatambuliwa kama hatua muhimu katika jenga Dunia yenye usawa. (Lengo la 4 Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa). Hususan, kuhakikisha ujumuishwaji ambao watoto wote wadogo wanapata fursa sawa ya kupata makuzi bora ya awali, malezi na elimu ni moja ya shabaha kuu za matokeo yaliyounganishwa na lengo hili. Sambamba na lengo hili, Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) ibara Na. 24 inayataka mataifa kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata fursa sawa ya elimu-jumuishi katika ngazi zote na kwamba uwe ni mchakato endelevu wa kujifunza maishani. Hili linaweza kufanyika kwa kuwezesha kupata njia mbadala za mawasiliano, kutoa afua stahiki, huduma za utengemao na wataalamu wa mafunzo ya elimu ya watu wenye ulemavu (UN, 2016). Ujumuishaji unalenga kutambua na kuheshimu haki za kila mtoto na hivyo, katika miaka ya mwanzo ya maisha yake kuonesha tofauti na kutazamwa kama kitu kizuri, na kutazamwa kama rasilimali nzuri ya umoja badala ya kuonekana kuwa jambo linaloleta shida (Booth, Nes, Stromstad, 2003). Utafiti unaonesha kuwa hatua ya mwanzo ya maisha siyo tu muhimu kwa ukuaji wa baadaye wa mtoto – bali inaweza pia kuwa muda mzuri kwa watoto kugundua tofauti kwa mtazamo mzuri. Kukubali tofauti ni muhimu kama tunataka kujenga jamii jumuishi na kupinga ubaguzi. Kwa upande mwingine, ujumuishaji ni wazo linalogombewa (Florian, 2014).

Kuongeza kwenye changamoto ya kutekeleza Elimu ya Makuzi ya Awali ya Mtoto (ECE) ni wazi kwamba, elimu jumuishi hailengi tu kwa watoto wenye ulemavu lakini pia inaangalia sifa zingine ambazo zinawafanya watoto wengine kuwa katika hatari ya kukosa fursa na haki ya elimu (mfano jinsia, kabila, umaskini). Elimu ya makuzi ya awali kwa mtoto inakusudia kukuza ukuaji mzuri wa mtoto, huku akihudumiwa malezi yake, na kupata mahitaji ya kielimu kwenye mfumo mkuu wa elimu (UNESCO, 2015). Kuelewa na kukubali wasifu na uwezo wa kipekee wa kila mtoto mapema na kutunga sera za kusaidia, kuweka mazingira jumuishi na fursa za kujifunza ni hatua muhimu katika kudumisha haki za watoto wote (Beecham na Rouse, 2012).




| | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| GER | 39.5 | 44.5 | 39.9 | 37.3 | 36.9 | 35.9 | 102.6 | 95.8 | 86.1 | 84 |
| NER | 37.5 | 42.4 | 41.8 | 35.5 | 33.4 | 33.3 | 46.7 | 44.6 | 39.9 | 38.7 |

Chanzo: BEST 2010 - 2019

Tanzania inatambua umuhimu wa ECE kama inavyooneshwa kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo (2014). Kwa utambuzi huu, elimu ya awali ni rasmi, inatolewa bure na ya lazima kwa watoto wote wenye umri wa miaka 4-5. Mwaka 2019, jumla ya shule za awali nchini Tanzania zilikuwa 17,771. Kati ya shule hizo, shule za serikali zilikuwa 16,155, sawa na asilimia(90.9) na shule binafsi zilikuwa 1,616 sawa na asilimia (9.1). Mwaka 2019, Wastani wa Uandikishaji kwa jumla (GER) ulikuwa 84.0% na Uandkishaji halisi (NER) ulikuwa 38.7%. Hii inamaanisha kuwa 61.3% ya idadi ya watoto wenye umri miaka 5 hawakuandikishwa elimu ya awali ambayo ni lazima. Wanaweza kuwa hawasomi kabisa au wameandikishwa shule za msingi.

Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) unahitaji serikali za mataifa kuhakikisha wanaweka mfumo wa elimu-jumuishi katika ngazi zote. Inalazimisha mataifa kuhakikisha kwamba sheria zao zinakuza haki za watu wenye ulemavu hasa kwenye elimu ambapo watoto wenye ulemavu wasome na wenzao kwenye shule jumuishi. Kwa maana hiyo, Ibara ya 24 ya mkataba wa haki za watu wenye ulemavu (CRPD) inazitaka serikali za mataifa kuhakikisha watoto wenye ulemavu "hawatengwi kwenye mfumo mkuu wa elimu bila kujali ulemavu wao, na kwamba wanapata elimu ya msingi na sekondari iliyo bora, bila malipo na jumuishi kwa misingi sawa na wenzao wasio na ulemavu ndani jamii wanamoishi ". Aidha, mkataba huo unazitaka serikali kuhakikisha zinatoa afua stahiki na msaada kwa mtoto binafsi kulingana na mahitaji ya aina ya ulemavu wake akiwa anasoma kwenye mfumo wa kawaida wa elimu. Kupitishwa kwa CRDP kuliashiria mabadiliko kwenye elimu-jumuishi. Kamati ya Haki za Mtoto (CRC) inatetea zaidi kufanya marekebisho ya utendaji ulizoeleka shuleni, utoaji wa huduma za msaada kwa wanafunzi na mafunzo kwa walimu wa kawaida ili waweze kusaidia watoto wenye mahitaji tofauti tofauti ya kielimu. Kongamano la Kimataifa la Salamanca kuhusu Elimu Maalum lilizitaka serikali zote, ikiwemo Tanzania, kufuata kanuni ya elimu-jumuishi na kuandikisha watoto wote kwenye shule za kawaida kama suala la kisheria au kisera.

Tanzania imetia saini Miongozo ya elimu-jumuishi. Iliridhia elimu-jumuishi mwaka 1998 miaka michache baada ya Mkutano wa Salamanca, kupitia mradi wa majaribio wa UNESCO uitwao 'Mahitaji Maalum darasani' (Tungaraza, 2012, Kisanga, 2017). Mradi ulianza na shule mbili, ambazo ni Shule ya Msingi Kibasila na Wailes zilizoko Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam. Mwaka 2005, Jeshi la Wokovu na Chama cha Walemavu wa Akili Tanzania (TAMH) waliungana na serikali kusaidia elimu-jumuishi katika maeneo mengine ya mkoa. Elimu-jumuishi ina lengo la kuondoa vizuizi ndani ya mfumo wa elimu ambavyo vinawatenga watoto wenye mahitaji maalum ya kielimu wakiwemo watoto wenye ulemavu. Inahitaji shule, walimu na madarasa kubadilika ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu.

Ili kukuza na kuhimiza utendaji unaozingatia ujumuishi, Tanzania iliandaa miongozo mbalimbali, ikiwemo Mapitio ya Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa 2017-2021, na kuandaa rasimu ya mkakati wa 2018-2021. Madhumuni ya mkakati ulioanzishwa hivi karibuni ni kuimarisha mfumo wa elimu, kutoa njia zenye usawa, kujiunga na shule, kushiriki kikamilifu na fursa za kujifunza kwa watoto wote. Mkakati huo unapendekeza zaidi kutoa mafunzo kwa wasimamizi na walimu juu ya elimu-jumuishi, na usambazaji wa vifaa stahiki vya kufundishia na kujifunzia ili visaidie kuwezesha ufundisha na kujifunzaji na elimu ya ualimu. Licha ya juhudi za kukuza ujumuishaji hadi sasa, inakadiriwa kuwa chini ya 40% ya watoto wenye ulemavu wameandikishwa shule ya msingi, na chini ya 2% wameandikishwa kwenye program za elimu maalum (Njelesani, Couto, na Cameron, 2011).

Aidha, utafiti unaonesha kuwa ni 38% tu ya watoto wenye ulemavu wenye umri wa kwenda shule ya msingi ndio wanaosoma shule, na karibu 0.4% tu ya watoto wote wanaosoma shule walibainika kuwa na 'mahitaji maalum au ulemavu' (Lehtomaki, Tuomi, na Matonya, 2014). Pia, inaonekana watoto wenye ulemavu wamepuuzwa kwa kiasi kikubwa kwa kufikiwa na tafiti nyingi (Alisha, 2020), hasa kuchunguza maendeleo ya kikundi hiki ndani ya mfumo jumuishi wa ECE. Vivyo hivyo, HakiElimu na mashirika mengine yanayounda Mtandao wa AIAL yaligundua pengo hili la maarifa. Hivyo, ilikubaliwa kuwa masuala muhimu yaulizwe kupitia maswali haya, "Je! ni mambo gani ya kimuktadha na ya kitaasisi ambayo yanaathiri utekelezaji wa Elimu Jumuishi ya Watoto wa Awali nchini Tanzania?": hali ya ECE jumuishi Tanzania; mifumo ya kisheria na miongozo ya kisera ya ECE kote (Tanzania Bara na Zanzibar); kiwango cha ujumuishaji kwenye ECE nchini Tanzania (upatikanaji, kubaki shule na kuvuka madarasa na ushiriki); miundo iliyopo (ngazi ya juu ikiwa ni serikali /wizara na ngazi ya chini mifumo ya jamii. Maswali haya yaliulizwa huku yakiambatana na mapendekezo ya mabadiliko.

Mtaala wa elimu ya awali unalenga watoto wote wenye umri wa miaka mitano, pamoja na wale walio na mahitaji maalum. Watoto wenye umri wa miaka mitatu hadi minne wanaweza kuruhusiwa kuandikishwa shule za awali kama tathmini ya mapema inaonesha kuwa wako tayari kwenda shule. Viashiria vya utayari wa shule ni pamoja na uwezo wa kujitegemea; uwezo wa kujieleza; shauku ya mtoto kupenda shule na uwezo wa kuelewa maelekezo rahisi. Pamoja na mambo mengine, elimu ya awali inaundwa kwa mtazamo jumuishi, ikihimiza hitaji la kushughulikia mahitaji ya watoto, yakiwemo yale ya watoto wenye mahitaji maalum. Ili kufanikisha hili, Sera ya Kitaifa ya Huduma kwa watu wenye Ulemavu ya 2004, inasema wazi hitaji la utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu ambao unapaswa kufuatiwa na afua/usaidizi stahiki. Sambamba na sera hii, Taasisi ya Elimu Tanzania imeandaa mtaala wa ECE ambao unawataka walimu kufanya utambuzi wa mapema wa watoto wenye mahitaji maalum na kutoa afua stahiki. Ingawa elimu ya awali inahimiza ujumuishaji, haijulikani sana kuhusu kiwango ambacho kanuni za ujumuishi zinatafsiriwa kuwa vitendo. Kwa maana hiyo, HakiElimu iliratibu utafiti kwa niaba ya Mtandao wa AIAL kuchunguza upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto wenye ulemavu. Utafiti ulilenga kuangalia hali ya mazingira na mifumo ya kitaasisi ambayo inawazuia watoto wenye ulemavu kupata na kushiriki kikamilifu kwenye elimu jumuishi ya awali na kupendekeza njia za kuboresha fursa za elimu kwa watoto wenye ulemavu.

## 1.1 Malengo

Utafiti uliongozwa na malengo yafuatayo;

- Kuchunguza kwa jinsi gani sera zilizopo, mifumo na mazingira vinasaidia kuwajumuisha watoto wenye ulemavu kwenye mazingira ya elimu ya awali.
- Kufahamu idadi ya watoto wenye ulemavu walioandikishwa madarasa ya awali na wanajifunza katika mazingira jumuishi.
- Kufahamu wastani wa idadi ya watoto wenye ulemavu wanaovuka kutoka elimu ya awali na kujiunga elimu ya msingi.
- Kubainisha vikwazo vya kimazingira na kitaasisi vinavyowazuia watoto wenye ulemavu kuandikishwa shule na kushiriki kikamilifu kwenye elimu-jumuishi ya awali.
- Kupendekeza njia za kuboresha upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto wenye ulemavu

## 1.2 Dhana Muhimu na Fasili zake

- **Elimu ya awali**: inamaanisha elimu ya lazima, bila malipo kwa watoto wa miaka 4 - 5
- **Elimu Jumuishi**: Kwa muktadha wa utafiti huu elimu-jumuishi inamaanisha mfumo wa elimu ambao watoto wote wanapata nafasi ya kuandikishwa, kushiriki kikamilifu hadi kumaliza mwaka mmoja wa mzunguko wa elimu ya awali bila kujali wasifu, historia zao na tofauti za uwezo wao, bila ubaguzi kupitia kupunguza vikwazo vya kijamii, kimazingira na kitaasisi na kuongeza rasilimali zaidi. Hata hivyo, utafiti huu, umejikita kwenye ujumuishaji wa watoto wenye ulemavu walio na umri kati ya miaka 4 na 5 kwenye elimu ya awali.
- **Elimu jumuishi ya awali**: maana yake ni mpangilio wa elimu ya awali ambapo vizuizi vimeondolewa kuwawezesha watoto wenye ulemavu wanaosoma elimu ya awali kujifunza kikamilifu na kushiriki vyema kwenye mfumo wa shule.
- Madarasa/shule mchanganyiko: inamaanisha mazingira ambayo wanafunzi wenye ulemavu hujifunza pamoja na wenzao wasio na ulemavu, ambapo; msaada wa ziada unaweza kutolewa kuwasaidia kuendana na mtaala wa kawaida, na wakati mwingine inawekwa program elimu maalum ndani ya darasa.

- **Ulemavu**: kuhusiana na shule ya awali humaanisha kupoteza au kuwa na udhaifu unazuia kushiriki kikamilifu kwenye mfumo wa elimu ya awali kwa kiwango sawa na wengine kwasababu ya udhaifu huo wa viungo, akili au vikwazo vya kijamii.
- **Mtoto mwenye ulemavu**: Katika muktadha wa utafiti huu mtoto mwenye ulemavu inamaanisha mtoto mwenye umri wa kwenda shule ya awali (mwenye umri wa miaka 4 - 5) aliye na ulemavu wa viungo, afya ya akili, hisia au kuelewa ambaye uwezo wake wa kufanya kazi unakuwa mdogo kutokana na vikwazo vya kimtazamo, mazingira na shule.

- **Upatikanaji**: inamaanisha kuwezesha au kumruhusu mtoto wa shule ya awali mwenye ulemavu kupata fursa mbali mbali za kujifunza, kushiriki shughuli, na kuyafikia mazingira katika muktadha wa elimu ya awali
  - **Ushiriki**: Baadhi ya watoto watahitaji afua stahiki na huduma saidizi binafsi ili kushiriki kikamilifu kwenye michezo na kujifunza wakiwa na wenzao na watu wazima.
  - **Misaada**: mifumo ya miundombinu ya misaada na huduma stahiki lazima iwepo ili kuimarisha juhudi za watu binafsi na mashirika yanayotoa huduma-jumuishi kwa watoto na familia.

## 1.3. Nadharia ya Wazo la Utafiti

### 1.3.1. Mitazamo ya mifumohali kwa ajili ya malezi na elimu jumuishi ya awali

Utafiti huu umeongozwa na mtazamo wa mfumohali wa malezi, makuzi na maendeleo ya aswali ya mtoto na elimu jumuishi ya awali. Mtazamo unazingatia ushawishi mpana kwa watoto unaotokana na mwingiliano wao kwa wao na uhusiano kati yao na mifumo inayowazunguka – mifumo midogo, ya kati, ya nje na mikubwa - ambayo hufanya kazi na kukua. Mtazamo huo unatoa fursa ya kuelewa nini kinaunda elimu bora jumuishi ya awali kuanzia ngazi ya matokeo-mchakato-muundo. Matokeo au lengo kuu na kipimo cha ubora wa elimu jumuishi ya awali ni kiwango cha ushiriki wa kila mtoto kwenye mazingira ya kijamii na ya kujifunza. Ushiriki wa mtoto unawezeshwa kupitia miundo jumuishi inayomzunguka ambayo hufanya kazi katika kiwango cha mifumo midogo midogo ambayo inajumuisha mazingira, miundombinu, jamii, tamaduni na elimu.

Kwa kawaida, kinachotokea kwenye ngazi ya mfumo-mdogo huathiriwa na sababu za muundo kwenye mfumo ngazi ya kati, ikitoka kwenye jamii ambako mazingira ya ujumuishwaji yamewekwa. Kinachotokea kwenye mazingira ya ujumuishwaji huathiriwa zaidi na masuala ya kimuundo ya mbali zaidi kwenye mfumo ngazi ya juu. Hii ni pamoja na uwepo wa sera, mifumo ya kisheria na ubora wa mitaala katika ngazi mbali mbali. Katika muktadha wa utafiti huu, mtazamo wa mifumohali hutumika kama mfumo wa uchambuzi, ambao uliwezesha kuelewa kwa kina elimu-jumuishi ya awali kuanzia ngazi ya sera hadi utendaji ndani na kwenye mifumo midogo midogo.

# 2. Mbinu za Utafiti

## 2.1 Maeneo ya Utafiti na Washiriki

### 2.1.1 Mikoa

Utafiti ulifanywa kwenye mikoa kumi; Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Tabora, Shinyanga, Kagera, Mtwara, Njombe, Kilimanjaro na Tanga. Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, na Tabora ilichaguliwa kwa makusudi kulingana na historia yao ya muda mrefu ya kuanzisha shule za watoto wenye ulemavu. Kwa mfano, shule mbili za kwanza maalum za watoto wenye ulemavu wa kuona, zilianzishwa mikoa ya Dodoma na Tabora miaka ya 1950 na 1962. Pia, Dar es Salaam ilikuwa mkoa wa kwanza kuanzisha shule jumuishi inayoweza kuchukua watoto wenye ulemavu wa kuona kwenye shule ya kawaida mwaka 1963, na mwaka 1984 ilianzisha shule maalum ya kwanza ya watoto wenye ulemavu wa akili. Pamoja na hayo, Dar es Salaam ilikuwa mkoa pekee wa kuendesha shule jumuishi kama utafiti wa majaribio mwaka 1997 na 2002. Mkoa wa Shinyanga ulishiriki kwenye utafiti huu kwasababu ya mauaji ya watu wenye ualbino miaka iliyopita. Mkoa huo ulikuwa wa muhimu kuchunguza wanajamii na utekelezaji wa elimu jumuishi. Mikoa ya Kagera, Lindi, Tanga na Kilimanjaro ilichaguliwa kinasibu kushiriki kwenye utafiti. Pia, uchaguzi wa mikoa ulizingatia maeneo ya kikanda za elimu kwa uwakilishi wa kijiografia: Kanda ya Kusini (Mkoa wa Lindi), Kanda ya Kati (Mikoa ya Dodoma na Tabora), Kanda ya Ziwa (Mkoa wa Kagera), Kanda ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro), Kanda ya Mashariki (Mkoa wa Dar es Salaam) na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mikoa ya Mbeya na Njombe). Uchaguzi wa mikoa kulingana na maeneo ya kikanda ulitokana na hitaji la uwakilishi wa kijiografia na uelewa kamili wa mada inayofanyiwa utafiti kutoka kwenye maeneo yenye utofauti, kitamaduni na kiuchumi.

### 2.1.2 Wilaya

Jumla ya wilaya 20, ambapo wilaya mbili kutoka kila mkoa ulioshiriki zilichaguliwa kushiriki kwenye utafiti. Watafiti, kwa kushirikiana na Maafisa Elimu wa Mkoa, walichagua wilaya zilizo na viwango vya juu na vya chini katika utekelezaji wa elimu jumuishi. Wilaya zilichaguliwa kinasibu

### 2.1.3 Shule

Jumla ya shule 80 zilichaguliwa kushiriki kwenye utafiti huu. Shule nne zenye madarasa ya awali zilichaguliwa kutoka kila wilaya iliyoshiriki. Hivyo, jumla ya shule 72 za umma na 8 binafsi zilishiriki katika utafiti huu. Kati ya madarasa yaliyochaguliwa, 11 yalikuwa madarasa mchanganyiko, 65 jumuishi na madarasa 4 ya kawaida. Lengo lilikuwa ni kuchunguza utekelezaji na mwenendo wa madarasa kutoka kwenye makundi tofauti ya shule/madarasa. Watafiti, kwa kushirikiana na maafisa elimu wa wilaya, walichagua shule mbili zenye kiwango cha juu na shule mbili zenye kiwango cha chini kwenye utekelezaji wa elimu jumuishi. Kujumuishwa kwa shule za binafsi kulitegemea upatikanaji wake ndani ya wilaya husika. Hivyo, shule 80 zilichaguliwa kushiriki kwenye utafiti huu.

### 2.1.4 Washiriki na utaratibu wa Kuwachagua

Jumla ya washiriki 1, 238 katika ngazi mbalimbali walihusika kwenye utafiti huu. Hawa ni pamoja na maafisa kutoka Wizara ya elimu na taasisi wakala wanaohusika na elimu ya awali na elimu-jumuishi. Aidha, utafiti huo ulijumuisha washiriki kutoka ngazi za mkoa, wilaya, kata, shule na jamii. Jedwali la 1 linaonesha washiriki kwa ngazi

**Jedwali 1: Idadi ya Washiriki kwa ngazi**

| | | |
|---|---|---|
| Maafisa Ngazi ya Kitaifa | Maafisa 4 kutoka Wizara ya Elimu (Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Afisa 1 mratibu wa elimu ya awalina afisa 1 kutoka kitengo cha elimu maalum), maafisa 4 kutoka OR-TAMISEMI, maafisa 2 kutoka TIE (Mkurugenzi wa Mitaalana Afisa 1 anayeratibu elimu ya awali), watu 2 kutoka Baraza la Watu wenye Ulemavu. | 14 |
| Maafisa ngazi ya Mkoa | Maafisa Elimu Mkoa (REO) 10, na Maafisa Elimu Maalum Mkoa 10 | 20 |
| Maafisa ngazi ya Wilaya | Maafisa Elimu Wilaya (DEO) 20, Maafisa Elimu Taaluma (DAO)-20, na Wathibiti ubora wa Shule 20, Maafisa Elimu maalum 20, Maafisa ustawi wa jamii/wataalam wa tiba 20 | 100 |
| Maafisa ngazi ya kata na vijiji | Maafisa Elimu Kata (WEO)-80, Maafisa Watendaji wa Kata (WEC)- 80, na Watendaji wa vijiji (VEO)-80 | 240 |
| Ngazi ya Shule na Jamii | Wakuu wa shule 80, Wenyevit wa kamati za shule 80, Walimu wa awali 77, wazazi 507-wenye watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu(angalau 6 kutoka kila shule iliyoshiriki utafiti) | 744 |
| **Jumla** | | **1118** |

## 2.2 Mbinu za Kukusanya Takwimu

Utafiti ulitumia mbinu za ukusanyaji wa takwimu za kiidadi na kiubora. Mbinu hizi ni pamoja na: uchambuzi wa maudhui kwenye nyaraka, mahojiano ya kina na watoa taarifa muhimu, majadiliano ya vikundi, ukaguzi darasani na mahojiano baada ya ukaguzi. Jedwali la 2 linaonesha lengo la utafiti na mbinu yake iliyotumika kukusanya takwimu.

**Jedwali 2: Lengo la utafiti, Uelewa na mbinu ya kukusanya data**

| Lengo la Utafiti | Uelwa wa timu wa lengo | Mbinu ya kukusanya data |
|---|---|---|
| 1. Chunguza jinsi sera na mifumo iliyopo inavyosaidia utoaji wa Elimu Jumuishi ya awali. | Tunaelewa kuwa lengo hili linakusudia kuleta uelewa wa sera, sheria mifumo iliyopo ya kitaifa na kijamii, na msaada unaotoa haki kwa wote, bila ubaguzi, kwa watoto wenye miaka 4/5 kuhudhuria na kushiriki elimu ya awali kwenye mfumo mkuu wa elimu. | 1. Uchambuzi wa maudhui ya nyaraka husika<br>2. Mahojiano ya kina na watoa taarifa muhimu<br>3. Uchunguzi shuleni na darasani<br>4. Mahojiano baada ya uchunguzi |

| | | |
|---|---|---|
| 2. Kufahamu uwiano wa idadi ya watoto wenye ulemavu walioandikishwa elimu ya awali na wanajifunza katika mazingira jumuishi | Tunaelewa kuwa lengo hili linakusudia Kupata taarifa ya asilimia ya watoto wenye mahitaji maalum wanaosoma shule na kushiriki kwenye mchakato wa kujifunza-kufunsishwa kwenye madarasa ya kawaida ya elimu ya awali. Aidha, lengo linakusudia kutoa uelewa wa mazingira wezeshi na vikwazo vinavyo wazuia baadhi ya watoto wenye mahitaji maalum kujiunga na shule za awali za kawaida. | 1. Mahojiano ya kina na watoa taarifa muhi<br>2. Madodoso |
| 3. Kufahamu idadi ya wanafunzi wenye ulemavu wanaopanda madarasa kutoka mazingira jumuishi (kutoka elimu ya awali kwenda shule ya msingi) | Tunaelewa kuwa lengo hili linakusudia kutoa uelewa wa idadi ya watoto wenye mahitaji maalum wakiwemo wenye ulemavu wanaopanda madarasa(kutoka awali kwenda elimu ya msingi). Aidha, lengo linakusudia kutoa uelewa wa mazingira wezeshi na vikwazo vinavyo wazuia baadhi ya watoto wenye mahitaji maalum kuvuka elimu ya awali na kujiungana shule za msingi. | 1. Mahojiano ya kina na watoa taarifa muhimu<br>2. Uchambuzi wa maudhui ya nyaraka husika |
| 4. Kupendekeza njia za kuboresha upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto wenye ulemavu | Tunaelewa kuwa lengo hili Linakusudia kutoa mapendekezo ya kiutendaji juu ya jinsi ya kuboresha upatikanaji, ushiriki, kuhitimu elimu ya awali na kuvuka kuendelea na elimu ya msingi kwa watoto wenye mahitaji maalum. | 1. Mahojianao ya kina na watoa taarifa muhimu<br>2. Majadiliano katika vikund<br>3. Tafakari ya matokeo muhimu Pamoja utendaji mzuri uliobainika wa elimu jumuishi ya awali |

### 2.2.1 Uchambuzi wa Maudhui ya nyaraka

Nyaraka kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na shabaha zake, Katiba ya Tanzania, Sheria ya Elimu, Sheria ya Haki ya Mtoto ya 2009, Sera ya Maendeleo ya Mtoto, Sera ya Elimu na Mafunzo (2014), Program za maendeleo sekta ya elimu(ESDP) za 2017/2018-2020/2021, - Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano wa Mwaka 2016/2017- 2020/2021 na Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi Tanzania zilichukuliwa na kufanyiwa uchambuzi wa maudhui yake. Nyaraka zingine zilizofanyiwa uchambuzi ni pamoja na nyaraka za mitaala ya elimu ya awali, (mtaala, silabasi, kiongozi cha mwalimu na vitabu vya kiada), kitabu cha viwango vya taaluma kwa walimu wa ECE na vitabu vya usajili wa wanafunzi wa darasa la awali.

### 2.2.2 Mahojiano ya kina na Watoa taarifa muhimu na Majadiliano ya vikundi

Mahojiano ya ana kwa ana yalifanyika kwa maafisa waliochaguliwa kutoka Wizara ya elimu (MoEST), OR-TAMISEMI na maofisa wa TIE, maafisa wa mkoa, wilaya, na vijiji, wathibiti ubora wa shule, maafisa ustawi wa jamii, maafisa elimu kata, watendaji wa kata, wakuu wa shule, walimu wa awali na wenyeviti wa kamati za shule. Jumla ya wazazi 507 (33% Me, 67% Ke) walishiriki kwenye majadiliano ya vikundi mjadala, wazazi 9.1% walitoka shule binafsi wakati wazazi 90.9% walitoka shule za serikali. Wazazi 62.3% waliripoti kuwa wana mtoto mwenye ulemavu.

Jumla ya majadiliano katika vikundi mjadala 75 vilifanyika kwa wazazi, kati ya hivyo 8 vilifanywa na wazazi kutoka shule binafsi wakati 67% walikuwa wazazi kutoka shule za umma. Na kila kikundi mjadala kiliundwa na angalau wazazi sita kutoka shule zilizochaguliwa. Vikundi vyote vilivyoundwa vilikuwa na wazazi wenye sifa mchanganyiko, wanaume na wanawake, na wazazi wa watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu. Mahojiano na Vikundi Mjadala viliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili inayozungumzwa na kueleweka na wengi, na vile vile Kiswahili ndiyo lugha ya kufundishia katika shule za msingi za umma nchini Tanzania. Mahojiano yalidumu kwa dakika 45 hadi saa moja na yalirekodiwa kwa sauti. Kurekodi kulisaidia sana kuhifadhi maneno ya washiriki na kuyarejea baadaye wakati wa uchakataji wa data na uandishi wa ripoti.

### 2.2.3 Madodoso

Madodoso yalijazwa na baadhi ya walimu wa awali waliochaguliwa. Dodoso lilitaka maoni na uzoefu wa washiriki juu ya uendeshaji na utekelezaji wa elimu-jumuishi ngazi ya awali. Aidha, dodoso lilichunguza taarifa zinazohusiana walimu wa shule ya awali, kuhusu maarifa yao, ujuzi wa kufundisha, mtazamo na motisha ya kufundisha watoto wenye mahitaji maalum katika mazingira jumuishi, vile vile kufahamu mahitaji yao ya uendelezaji wa taaluma. Mfumo wa programu mtandao, uitwao 'Mobenzi', ulitumiwa kuwezesha ukusanyaji wa takwimu za kiidadi, ulisaidia ukusanyaji wa data kwenye vifaa vya Android (simu na Vishkwambi). Madodoso yalibadilishwa na kuwekewa alama tambulishi kwenye mfumo.

### 2.2.4 'Uchunguzi wa desturi za watu na mahojiano baada ya uchunguzi

Uchunguzi na ukaguzi wa shule na darasani ulifanyika. Pamoja na mambo mengine, uchunguzi uliangalia masuala yanayohusiana vitendo vya ufundishaji, vifaa vya kufundishia-kujifunzia na zana mbalimbali vile vile uliangalia miundombinu ya shule. Uchunguzi ulifanywa wakati wa kipindi kamili cha darasa la awali ukiongozwa na ratiba ya ukaguzi. Mahojiano baada ya uchunguzi yalifanywa na wakuu wa shule na walimu wa awali ili kukazia taarifa zilizokusanywa. Mahojiano haya yalifanywa punde tu baada ya kukamilisha uchunguzi.

## 2.3 Usimamizi, Uchakataji na Uchambuzi wa data

### 2.3.1 Data kutoka kwenye mahojiano, vikundi mjadala na uchunguzi

Uchambuzi wa taarifaza kiubora ulikuwa wa kujenga nadharia na kufanyia majaribio ya nadharia zilizopo. Takwimu hazikuchukuliwa kutokana na nadharia zilizokuwepo kabla bali zilichukuliwa kuendana na uhalisia. Kwa maana, uelewa mpana zaidi wa jambo ambalo linachunguzwa utachangiwa na vyote- malengo/maswali ya utafiti na taarifa zinazoibuka kutoka kwenye data. Hata hivyo, hatua tatu kuu ziliongoza uchambuzi wa data za kiubora: kuandaa na kuzipanga vizuri data, kupanga makundi /maudhui ya data, kuweka alama tambulishi, kuwasilisha na kutafsiri.

Maandalizi na upangaji wa taarifa kwa ajili ya uchambuzi vilianza tukiwa kwenye maeneo ya utafiti. Hii ilihusisha kusikiliza mahojiano yaliyorekodiwa kutoka kwenye mahojiano ya watoa taarifa muhimu na majadiliano ya vikundi mjadala, kisha ikafuatiwa na zoezi la kuyaweka (kuyaandika) mahojiano hayo kwenye maandishi. Baada ya hapo, maudhui yalitolewa kutoka kwenye maswali ya utafiti, na kisha kuyahusianisha na malengo ya utafiti. Mbinu ya kujenga nadharia ilihusisha kusoma maandishi ya muswada wa utafiti kwa kurudia rudia ili kutambua maandishi yanayohusika na kutoa tafsiri. Hatua ya tatu ilihusisha kuweka alama tambulishi, uwasilishaji na ufafanuzi wa matokeo. Taarifa zilizoandikwa kutoka kwenye kinasa sauti zilisomwa tena ili zipewe alama tambulishi, ambayo ilihusianisha data na maudhui yaliyotengenezwa. Hii ilikuwa ni kazi ya kubainisha vipengee vya maandishi - maneno, sentensi, na, au aya - kutoka kwa kila maandishi yaliyochapwa, na kuviweka kila kipengele kwenye mada/ maudhui inakohusiana. Aidha, mtafiti huru alipitia dondoo zote za taarifa zilizo na alama tambulishi kwa kila mada/maudhui. Hii iliwawezesha watafiti kufanya upya na kurekebisha mada/maudhui na dondoo zinazohusiana.

### 2.3.2 Usimamizi wa Taarifa za kiidadi na mipango ya uchambuzi

Timu ya utafiti ilihakikisha kuwa daftari lenye ubora wa juu la dataseti/kanzidata iliyosafishwa linakuwepo. Zoezi hili lilianzia maeneo ya utafiti na kuendelea hadi mwisho wa mchakato wa kukusanya data. Takwimu zilisafishwa na kukaguliwa kwa uangalifu kuona makosa, usahihi, kubaini na kushughulikia vipengele vilivyorukwa au kukosekana. Kukagua data kulijibu maswali kama vile data zinasomeka? Je, majibu yamekamilika? Maswali muhimu yamejibiwa? Je, taarifa zote za kimazingira zimejumuishwa (kwa mfano, takwimu, muda, mahali)? Takwimu Elezi kama idadi ya kutokea, asilimia, na wastani zilifanyiwa kazi na kuwasilishwa kwenye kwenye majedwali na chati.

## 2.4 Hatua za kudhibiti ubora

Ubora wa utafiti huu ulitokana na kuweka mipango yenye tija na inayotekelezeka, taratibu makini za kuajiri, mafunzo ya timu ya utafiti, majaribio ya zana za utafiti na kufanya marekebisho ya zana za kukusanyia data. Wahojaji walipewa itifaki ya ukusanyaji wa takwimu ili iwaongoze kwenye ukusanyaji watakwimu kila siku;pia usimamizi wa karibu kusaidia wahojaji kwenye masuala ya kiufundi kuhusu kuhusisha zana za kukusanya takwimu mtandaoni kupitia kishakwambi, vile vile kulikuwa na Wahojaji viongozi na Wasimamizi. Waliofanya ukaguzi na uhakiki wa ubora wa shughuli zote za ukusanyikataarifa na takwimu kupitia kuangalia uendeshaji mahojiano, kufanya vikao vifupi kila siku kupata mrejesho wa yaliyojiri siku nzima na kukubaliana namna nzuri ya kusonga mbele.

## 2.5 Kuzingatia Maadili ya utafiti na kuwalinda washiriki

Washiriki walijulishwa lengo na aina ya utafiti kabla ya mahojiano, pia walijulishwa faida zinazoweza kupatikanaa kutokana na utafiti huu, na haki zao za kushiriki au kukatisha ushiriki wao muda wowote wanapojisikia kufanya hivyo. Pia waliambiwa kuwa taarifa watakazotoa zitakuwa siri na kwamba taarifa hiyo haitahusianishwa na utambulisho wao kwa namna yoyote. Baada ya hapo, washiriki waliombwa kutoa ridhaa kamili ya kushiriki kwenye utafiti. Watoto walipewa maelezo rahisi na ridhaa iliombwa kwa wazazi, walezi au wakuu wa shule, kuendana na Sera ya Kulinda Mtoto.

# 3. Matokeo ya Utafiti

## 3.1 Mazingira ya Sheria na Sera

### 3.1.1 Sheria na Sera

Uchambuzi wa nyaraka za sera unaonesha kuwa Tanzania ina mfumo mzuri wa kisheria unaowahakikishia haki za watu wenye ulemavu katika mazingira mbalimbali. Hii inaungwa mkono na uamuzi wa Tanzania kusaini miongozo mbalimbali ya kimataifa inayotetea na kulinda haki za watu wote pamoja na wale wenye ulemavu. Kwa mfano, Tanzania imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (1989), ambao unasisitiza haki za watoto kupata elimu, ili kufikia ujumuishi wa kijamii, pamoja na mambo mengine.

Vivyo hivyo, Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu linahimiza serikali kuhakikisha kwamba wasichana na wavulana wote wanapata usawa katika malezi na makuzi bora ya utotoni, matunzo na elimu ya awali ifikapo mwaka 2030. Hapa Tanzania, kanuni ya haki sawa ya elimu imebainishwa kwenye sera, miongozo na sheria mbalimbali (mifano; Sheria ya Elimu, ya 1978; Sera ya Elimu na Mafunzo, ya 1995; Sera ya Maendeleo ya Mtoto, ya 1996; Sera ya Taifa ya Huduma kwa watu wenye Ulemavu, ya 2004; Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, ya 2010; Sera ya Elimu na Mafunzo, ya 2014).

Sheria ya Watu wenye Ulemavu, 2010, inahimiza huduma za afya, msaada wa kijamii, maeneo kupitika na kufikika, huduma za utengemao, elimu na mafunzo ya ufundi, mawasiliano, ajira au uhakika wa kazi na kukuza haki za msingi kwa watu wenye ulemavu. Sheria inasema kuwa watu wenye ulemavu kwa kila rika na jinsia watakuwa na haki sawa ya kupata elimu, mafunzo katika mazingira jumuishi na manufaa ya tafiti kama wananchi wengine. Aidha, Sheria inasisitiza kuwa kila mtoto mwenye ulemavu atakuwa na haki sawa za kuandikishwa kwenye shule za umma au za binafsi.

Pamoja na hayo, Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) inasisitiza juu ya upatikanaji sawa na ushiriki wa watoto wote kwenye elimu ya msingi ya lazima na bila malipo kama msingi wa kupata elimu zaidi, sera hiyo inabainisha utekelezaji wa elimu ambao unachukua wanafunzi katika mfumo mzima wa elimu ambao utahakikisha hakuna kutengwa kwa mtoto yeyote. Sera za Kitaifa zimetafsiriwa katika mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kitaifa na sekta ya elimu. Kama ilivyoelezwa mahali pengine, Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi ulioandikwa hivi karibuni 2018-2021, kwa mfano, unasisitiza juu ya hitaji la kuhakikisha

- Upatikanaji sawa na ushiriki katika elimu ikiwemo angalau mwaka mmoja wa elimu ya awali unaimarishwa kwa watoto wote wa miaka 5 na hasa kwa makundi yenye mazingira magumu na yaliyotengwa.
- Wanatoa mafunzo kwa viongozi na waalimu juu ya utambuzi wa mapema na kuboresha mfumo wa kuchunguza na kuchagua watoto wa umri wa elimu ya awali.
- Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya elimu ya awali ambavyo vinawaandaa walimu kwa ajili ya kufundisha elimu-jumuishi ya awali. Jedwali la 3 ni muhtasari wa sheria /sera zinazohusiana na watu wenye ulemavu.

**Jedwali la 3: Sera na Sheria kuhusu watoto wenye ulemavu na elimu**

| Sheria/Sera | Kifungu Cha Sheria/Sera |
|---|---|
| 1. Sheria ya Mtoto ya 2009 | • Elimu inapaswa kupatikana kwa kila mtoto kupitia njia za vitendo zaidi ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vya kusaidia watoto wenye mahitaji maalum ya elimu na wale wenye ulemavu…… |
| 2. Mkakati wa itafia wa Elimu Jumuishi (2009-2017) | Umelenga kuhakikisha kwamba:<br>• Sera na mipango ya elimu vinaongozwa na kanuni na matendo jumuishi<br>• Ufundishaji na ujifunzaji unakidhi mahitaji tofauti tofauti ya wanafunzi<br>• Uwezo wa kitaalam kwa ajili ya elimu jumuishi unapanuliwa na kuimarishwa |
| 3. Sheria ya Watu wenye ulemavu (2010) | Inasema kwamba,<br>• Watu wenye ulemavu katika umri wowote na jinsia watakuwa na haki sawa za kupata elimu, mafunzo katika mazingira jumuishi na kunufaika na tafiti kama wananchi wengine<br>• Kila motto mwenye ulemavu ana haki sawa ya kuandikishwa shule za serikali au shule binafsi |
| 4. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 | Inatetea na kuhimiza:<br>• Matumizi ya lugha ya lama na maandishi ya nukta nundu kwenye ngazi zote za elimu.<br>• Kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa watoto wote wakiwemo wenye ulemavu<br>• Kuhakikisha miundombinu yote muhimu inajengwa mazingira ya shule ili iwafae wanafunzi wote |
| 5. Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (2016/17-2020/21 | Unahimiza<br>• Watoto wenye ulemavu kujumuishwa kwenye mfumo mkuu wa elimu, na shule maalum kwa wale ambao wana ulemavu mkubwa<br>• Kuwepo na mpango wa kufanya utambuzi wa mapema kuangalia ulemavu wa watoto.<br>• Inahimiza wanafunzi wenzao kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu mdogo |
| 6. Mtaala na Silabasi ya Elimu ya awali (2016) | Moja ya malengo ya elimu ya awali ni<br>• Kutambua watoto wenye mahitaji maalum na kutoa afua/usaidizi stahiki<br>• Inazingatia kanuni za ujumuishi maana inashughulikia mahitaji ya watoto wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum<br>• Inahimiza kufundishwa mwanafunzi binafsi Inasisitiza juu ya kukuza haki na wajibu wa mtoto |
| 7. Mapendekezo ya kupitia upya fomula ya kugawa ruzuku ya wanafunzi MoEST na OR-TAMISEMI (2017) | • Kuboresha haki ya mgaw wa Ruzuku ya Wanafunzi kwa kuzingatia idadi ya watoto wenye mahitaji maalum ya elimu shuleni.<br>• Kutoa rasilimali za ziada kugharamia mahitaji ya elimu maalum shuleni shule |
| 8. Mkakati mpya wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi (2018-2021) | • Imarisha mfumo wa elimu ili kutoa, kwa usawa, fursa za kujifunza kwa watoto wote<br>• Upatikanaji na ushiriki sawa kwa angalau mwaka mmoja wa elimu ya awali uimarishwe kwa watoto wote wa miaka 5 na hasa kwa watoto wanotokea kundi la waishio katika mazingira magumu<br>• Kutoa mafunzo kwa viongozi na waalimu juu ya utambuzi wa mapema na kuboresha mfumo wa uchunguzi wa watoto wenye umri wa kusoma elimu ya awali<br>• Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya awali ambavyo vinawaandaa walimu kwa ajili ya elimu-jumuishi ya awali |
| | |

### 3.1.2 Ujumuishi wa Mtaala na Zana za mtaala

Mtaala wa Elimu ya Awali na Silabasi/Muhtasari ya Masomo ya 2016 na zana za mtaala imetokana na kanuni ya elimu-jumuishi. Mtaala huo unakusudia kumuwezesha kila mtoto kukuza umahiri na wezo ambao utamsaidia kupata mahitaji yake ya kielimu na makuzi. Mtaala unatokana na kanuni jumuishi kwani inashughulikia mahitaji ya watoto wote pamoja na wale wenye mahitaji maalum kwa kuwezesha ukuaji wao na uwezo wa kufanya vitendo maalum. Moja ya malengo ya elimu ya awali ni kutambua watoto walio na mahitaji maalum na kuwapatia msaada stahiki. Pamoja na hayo, Mtaala unazungumzia pia masuala mbalimbali mtambuka, na kukuza haki za, na majukumu ya mtoto. Masuala mtambuka yamejumuishwa katika umahiri unaotarajiwa, na yanaonekana katika shughuli mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji.

Mtaala wa elimu ya awali unazidi kusisitiza uwepo wa walimu wenye mafunzo stahiki na angalau walimu wawili kwa kila darasa la awali. Uwiano uliopendekezwa wa mwalimu na mtoto ni 1:25. Kwa upande wa rasilimali zisizo za kibinadamu, utekelezaji mzuri wa mtaala unategemea upatikanaji wa miundombinu ya kutosha na inayofaa kwa watoto, samani, na zana za kufundishia, ambazo zinauwezo wa kukidhi mahitaji ya watoto wote pamoja na wale wenye mahitaji maalum. Mtaala pia unatoa wito wa mafunzo endelevu ya kukuza ujuzi wa kitaalam kwa waalimu kupitia njia mbalimbali ikiwemo ujifunzaji wa ngazi ya shule kwa waalimu wanaofundisha madarasa ya awali. Katika kuendeleza kipengele hiki, Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) kwa kushirikiana na wadau wengine ilitengeneza moduli sita za kusaidia kutekeleza mafunzo hayo ya ngazi ya shule. Moja ya mada katika moduli hizo inalenga kukuza uwezo wa walimu wa elimu jumuishi ya awali.

#### 3.1.2.2 Vitabu vya Kiada

Mtaala na muhtasari wa masomo ya Elimu ya Awali vinasisitiza kuwa; vitabu sita vya kiada na vitabu vya hadithi kumi na mbili vinatarajiwa kupatikana kwa kila mtoto darasa la awali. Sambamba na hilo, vifaa saidizi vinatakiwa kuwepo shuleni kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu kujifunza. Hata hivyo, utafiti huu uligundua upungufu mkubwa wa vitabu vya kiada, vitabu vya hadithi na zana za kuwasaidia watoto wenye ulemavu. Hili liliripotiwa na washiriki wengi na ilionekana katika shule zilizotembelewa. Vitabu vilivyokuwepo vilionekana vya rangi na ukubwa wa maandishi uliotumika unasomeka vyema na unafaa kwa watoto. Hata hivyo, hakukuwa na vitabu vya kiada au vitabu vya hadithi maalum kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watoto wenye ulemavu wanawakilishwa kwa kiasi fulani katika mada za vitabu vya kiada vya elimu ya awali. Ni vitabu viwili tu kati ya sita vinawakilisha watoto wenye ulemavu. Kwa mfano, katika kitabu cha kiada cha 'Kutunza Mazingira', kuna picha kwenye Ukurasa 18, inayoonesha mtoto mwenye ualbino, kwenye Ukurasa 32 picha ya mtoto mwenye uoni hafifu, wakati Ukurasa wa 35 kuna picha ya mtoto aliye na ulemavu wa viungo. Vivyo hivyo, kwenye kitabu cha kiada cha 'Kuhusiana na Wengine', kwenye ukurasa wa 22 picha inaonyesha mtoto aliye na ulemavu wa viungo na inaonyesha njia ya kupandia ili kufikia darasa kwa urahisi kwa watoto wenye ulemavu.

Uwakilishi mzuri wa watoto wenye ulemavu unapongezwa kwa sababu unasaidia kubadilisha mitazamo na kuvunja dhana potofu dhidi ya ulemavu. Hata hivyo, majengo yote yaliyoonyeshwa kwenye kitabu cha kiada hayaonyeshi njia za kupandia kuingia ndani zinazotumiwa na watoto wenye ulemavu wa viungo. Kati ya majengo yote 53 yaliyoonyeshwa katika vitabu vyote vya kiada, ni majengo mawili tu yanaonyesha njia za kupandia kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa viungo. Kitabu hicho kinaonyesha choo kilicho na ngazi maalum kwa walemavu wa viungo na macho.




*Picha ilichukuliwa kutoka kwenye kitabu cha kiada cha 'Kutunza Mazingira', ukurasa wa 22 ikionesha mtoto mwenye ulemavu wa viungo akiwa mazingira jumuishi*

Kutokana na uchambuzi wa sheria na sera, tunajifunza kuwa elimu ya awali nchini Tanzania haina ada katika shule za umma na ni ya lazima kwa watoto wote wenye umri wa miaka 4 hadi 5. Ni mpango wa mwaka mmoja wa kuandaa watoto kuingia elimu ya msingi. Hakuna shaka kuwa serikali ya Tanzania inatoa msaada mkubwa kwa elimu ya watoto wenye ulemavu katika ngazi zote. Sera na miongozo inatetea na kuhimiza upatikanaji sawa na ushiriki wa watoto wenye ulemavu katika mazingira jumuishi ya elimu ya awali.

Sera na miongozo ya serikali imejikita siyo tu kwenye uandikishaji wa watoto wenye ulemavu lakini pia iko wazi kwenye dhamira yake ya kuzifanya shule na madarasa kuwa jumuishi kwa watoto wenye ulemavu na kuweza kukidhi mahitaji yote ya wanafunzi. Sera na miongozo imeleza maana ya mtoto mwenye ulemavu. Hii ni muhimu kwa program ili kutimiza mahitaji ya watoto wanaosoma elimu ya awali. Kwa mfano, Mtaala na Silabasi za elimu ya Awali na Msingi za mwaka 2016, inahitimiza kufanya utambuzi wa mapema na kutoa afua stahiki kwa watoto wenye mahitaji maalum. Inasisitiza zaidi hitaji la kurekebisha mtaala na kubuni ufundishaji unaoendana na mahitaji binafsi ya mtoto ili kuwawezesha watoto kuhudhuria na kushiriki kikamiifu kwenye mchakato wa kufundisha na kujifunza.

## 3.2 Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu elimu ya awali

Uchambuzi watakwimu unaonesha kuwa uandikishaji ngazi ya elimu ya awali unabadilika badilika. Hii ni sawa na uandikishaji ngazi ya taifa. Pengo la jinsia ni dogo sana. Watoto wenye umri wa miaka 5 wameonekana kuwa na zaidi ikilinganishwa na miaka mingine. Angalia Kielelezo cha 2.




| | 2016 Wav | 2016 Was | 2016 Jumla | 2017 Wav | 2017 Was | 2017 Jumla | 2018 Wav | 2018 Was | 2018 Jumla | 2019 Wav | 2019 Was | 2019 Jumla | 2020 Wav | 2020 Was | 2020 Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Walioandikishwa miaka 3 | 129 | 151 | 280 | 183 | 149 | 332 | 149 | 159 | 308 | 210 | 192 | 402 | 146 | 158 | 304 |
| Walioandikishwa miaka 4 | 573 | 630 | 1203 | 666 | 686 | 1352 | 764 | 783 | 1547 | 889 | 827 | 1716 | 695 | 673 | 1368 |
| Walioandikishwa miaka 5 | 1333 | 1474 | 2807 | 1476 | 1387 | 2863 | 1655 | 1584 | 3239 | 1798 | 1666 | 3464 | 1514 | 1475 | 2989 |
| Walioandikishwa miaka 6 | 734 | 643 | 1377 | 944 | 824 | 1768 | 727 | 656 | 1383 | 737 | 632 | 1369 | 843 | 682 | 1525 |
| Zaidi ya miaka 6 | 326 | 342 | 668 | 357 | 318 | 675 | 276 | 269 | 545 | 281 | 346 | 627 | 380 | 346 | 726 |

Kielelezo cha 2: Uandikishaji wa watoto wenye umri wa kujiunga na shule ya awali ki-umri kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020

**Chanzo: Data za utafiti**

Kielelezo 3 kinawasilisha idadi ya watoto wa shule za awali walioandikishwa mwaka 2020 kwenye madarasa ya awali tuliyotembelea, zikionesha kuwa watoto wa umri wa miaka 5 waliandikishwa elimu ya awali wengi zaidi mwaka 2020 ikilinganishwa na wenzao wenye umri wa miaka 6. Hii haishangazi, kwakuwa miaka 5 ni umri wa lazima mtoto kuandikishwa shule ya awali.




Kielelezo cha 3: Uandikishaji watoto elimu ya awali kwa umri wao, 2020

**Chanzo: Takwimu za utafiti**

Kielelezo cha 4 kinaonesha ongezeko la 14% ya uandikishaji wa watoto wenye ulemavu shule za awali kwa ngazi ya taifa, ambayo iliongezeka kutoka watoto 3,713 mwaka 2,017 hadi watoto 4,240 mwaka 2,019. Hata hivyo, uandikishaji huo siyo wa mwendelezo, hubadilika badilika. Kwa mfano, mwaka 2018 ulishuka kwa 6.4% ikilinganishwa na uandikishaji wa 2017. Mwaka 2019, uliongezeka kwa 21.5% kutoka asilimia ya mwaka 2018. Vivyo hivyo, uandikishaji wa watoto kwa kuangalia makundi ya ulemavu hubadilika badilika.




Kielelezo cha 4:Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu madarasa ya awali kitaifa, 2017-2019

**Chanzo: Basic Education Statistics Tanzania (BEST), 2017, 2018 and 2019**

Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu ngazi ya taifa umegawanywa kwa aina ya ulemavu na jinsia. Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu wa viuongo na afya ya akili ulikuwa juu zaidi miaka miaka kadhaa ikilinganishwa na aina nyingine za ulemavu. Kwa mfano, mwaka 2019, uandikishaji wa watoto wenye ulemavu wa mwili na akili ulikuwa 34% na 24% mtaalia. Uandikishaji huu ulichukua 58% ya jumla ya uandikishaji wote. Ulemavu wa kuona ulikuwa na idadi ndogo zaidi. Ingawa data kuhusu watoto wenye ulemavu kwa umri hazikuwepo, mgawanyo wa uandikishaji kwa aina ya ulemavu na jinsia ni muhimu kwa mipango na program. 3.3 Mfumo wa uandikishaji wa watoto wenye ulemavu kwa mkoa, 2016-2020

## 3.3 Mwenendo wa Uandikishaji watoto wenye ulemavu Ki-mkoa kuanzia 2016 hadi 2020

Utafiti ulitaka kuelewa zaidi hali ya uandikishaji wa watoto wenye ulemavu kwa miaka mitano iliyopita na Ki-mkoa. *Kielelezo cha 5* kinaonesha mwenendo wa uandikishaji.




Kielelezo cha 5: Mwenendo wa Uandikishaji watoto wenye ulemavu Ki-mkoa kuanzia 2016 hadi 2020

**Chanzo: Takwimu za Utafiti**

Kielelezo cha 5 kinaonesha kwamba, ingawa kulikuwa na kupungua kwa wastani wa uandikishaji kuanzia mwaka 2017 hadi 2020, Mkoa wa Tabora ulirekodi uandikishaji wa juu zaidi kwa miaka hiyo ikifuatiwa na Mikoa ya Dar es Salaam na Lindi. Kwenye mikoa mingine, uandikishaji umekuwa mdogo miaka yote. Tofauti ya uandikishaji wa watoto wenye ulemavu kimkoa inaweza kuhusishwa na sababu kadhaa, zikiwemo mwamko wa jamii juu ya haki ya elimu kwa watoto wenye ulemavu na uwepo wa taratibu za kutambua watoto wenye ulemavu katika jamii.

**Kielelezo cha 6** kinaonesha mwenendo wa wanafunzi wenye ulemavu walioandikishwa madarasa ya awali kipindi cha mwaka 2016-2020. Watoto wenye ulemavu wa afya ya akili walirekodi mwenendo mkubwa zaidi wa uandikishaji wakati wenzao wenye ulemavu wa kusikia na kuona walikuwa na uandikishaji mdogo zaidi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.




**Kielelezo cha 6: mwenendo wa uandikishaji wa watoto wenye ulemavu mwaka 2016-2020 kwa kundi la ulemavu.**

**Chanzo: Takwimu za Utafiti**

Takwimu za uandikishaji wa watoto wenye ulemavu elimu ya awali ni zinatoa taarifa nzuri. Hata hivyo, hazioneshi idadi ya watoto wa shule ya awali, waliojiunga shule kulinganisha na idadi ya jumla ya watoto wote wenye umri wa kuandikishwa elimu ya awali. Hii inamaanisha kuwa takwimu za sasa hazioneshi asilimia ya watoto wenye ulemavu, ambao bado hawajaandikishwa shule ya awali.

Takribani shule zote, kata, wilaya na mikoa iliyotembelewa haina takwimu za kina na zilizounganishwa za watoto wenye ulemavu. Wanaweza kuwa na idadi ya wanafunzi wenye ulemavu waliojiunga na madarasa ya elimu ya awali lakini siyo kwa umri au aina ya ulemavu. Hakukuwa pia na takwimu kamili zinazohusiana na watoto wenye ulemavu wanaokamilisha elimu ya awali na kujiunga na elimu ya msingi katika ngazi za kata au wilaya. Maafisa watendaji wengi wa kata hawakuwa na takwimu zilizojumuishwa. Pamoja na hayo, matokeo ya utafiti kutoka kwenye jamii yanaonyesha kuwa hakukuwa na takwimu za idadi ya watoto wenye rika la kujiunga na elimu ya awali (miaka 4 na 5) wenye ulemavu au wasio na ulemavu katika ngazi za kata, wilaya na mkoa. Maafisa watendaji wa kata, maafisa elimu wa wilaya na maafisa elimu kata waliripoti kwamba mara nyingi waliwaomba viongozi wa vijiji kuwasaidia kubaini watoto wenye ulemavu na kutoa idadi yao katika vijiji husika, hata hivyo, takwimu zilipopatikana, hazikuwa katika namna ambayo ilitarajiwa.

Licha ya kuongezeka kwa uandikishaji wa watoto wenye ulemavu, hatuwezi kusema kuna mafanikio katika suala la uandikishaji elimu ya awali kwa kuwa hatujui asilimia ya wanafunzi waliojiunga na darasa la awali kati ya idadi ya watoto wenye ulemavu na wale ambao hawajaandikishwa shuleni. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa watoto wengine wenye ulemavu wana fursa ndogo ya kupata elimu ya awali. Takribani 29% ya wakuu wa shule hawakukubaliana na kauli ya kwamba watoto wenye ulemavu wana fursa sawa ya kupata elimu ya awali.

### 3.4 Kiwango cha kuhitimu & kuvuka darasa kwa watoto wenye ulemavu (awali kwenda darasa la I)

Takwimu kwa sehemu kubwa zimeshindwa kuonesha viwango vya kuvuka darasa watoto wenye ulemavu kutoka elimu ya awali kwenda shule ya msingi. Takwimu za ElimuMsingi ya Tanzania zinaonesha kuwa watoto wenye ulemavu wameandikishwa Darasa la I, na uandikishaji umekuwa ukiongezeka. Katika *kielelezo cha 7* hapa chini, kinaonesha mwenendo wa uandikishaji wa wanafunzi waliovuka kutoka elimu ya awali kwenda elimu ya msingi. Wanafunzi wenye ualbino wameonesha kiwango cha juu cha kuvuka darasa kwenda shule ya msingi kwa miaka kadhaa ikilinganishwa na wanafunzi wenye ulemavu mwingine. Uvukaji darasa wa wanafunzi wenye ulemavu wa kuona na kusikia umekuwa chini miaka yote.




**Kielelezo cha 7: Mwenendo wa Kuvuka darasa wa watoto wenye ulemavu**

**Chanzo: Kitabu cha Takwimu za ElimuMsingi Tanzania (BEST), 2016, 2017, 2018 na 2019**

Ingawa kuna ongezeko stahimilivu la asilimia (kutoka 54.8% mwaka 2014 hadi 78.6% mwaka 2019) ya watoto wanaoingia Darasa la kwanza wakiwa wamepitia eimu ya awali, Takwimu za uandikishaji wa watoto wenye ulemavu kuingia Darasa la I (Tazama **Kielelezo cha 8**) hazina taarifa ya kutosha kuonesha kwamba wanafunzi walioandikishwa walisoma darasa la awali.




Kielelezo cha 8: Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu.

**Chanzo: Data za Utafiti**

## 3.5 Mambo yanayozuia watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali

Mambo mbalimbali yaliripotiwa na wahojiwa kuwa ni vikwazo kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali, vikwazo hivyo vinaanzia ngazi ya familia, shule na jamii. Kwa mfano, walimu wakuu wengi (71%), waliripoti kwamba wazazi wana mtazamo kwamba watoto wenye ulemavu hawawezi kujifunza. Mtazamo huu uliwashawishi wazazi kutowaandiskisha shule watoto wenye ulemavu. Karibu 57% ya wakuu wa shule waliripoti kuwa kuna unyanyapaa dhidi ya watoto wenye ulemavu na dhidi ya familia ndani ya wanajamii. Matokeo yake, wazazi walikuwa wanawaficha watoto wao nyumbani. Matokeo ya utafiti yanaonesha zaidi kuwa 57% ya wakuu wa shule zilizotembelewa waliripoti kuwa watoto wenye ulemavu, hasa wale wenye ulemavu mkubwa walikataliwa kuandikishwa shule na hivyo kunyimwa fursa ya elimu ya awali. Kielelezo cha 9 kinatoa kwa muhtasari wa mambo yanayozuia watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali.




**Kielelezo cha 9: Mambo yanayozuia watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali**

**Chanzo: Takwimu za utafiti**

Sababu hizi zinaweza kugawanywa katika makundi makubwa matatu; **jamii, shule na kijiografia**. Zilipo changanuliwa kiidadi, sababu za kijamii zilizidi kwa mbali sababu zingine, zikichukua 67% wakati mazingira ya shule 22% na vikwazo vya kijiografia zinachukua 11%.

Sababu zinazowazuia watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali zilisisitizwa na washiriki wakati wa mahojiano na majadiliano ya vikundi mjadala. Sababu hizo ni pamoja na unyanyapaa dhidi ya watoto wenye ulemavu na familia zao na athari zinazohusiana na hilo, utashi wa wazazi kuwaandikisha watoto wao wenye ulemavu kwenye shule maalum badala ya shule jumuishi, umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shule na uhaba wa rasilimali za kugharamia huduma na vifaa stahiki kwa watoto wenye ulemavu wakiwa shule za kawaida

### 3.5.1 Unyanyapaa dhidi ya watoto wenye ulemavu na familia zao

Baadhi ya wanajamii katika maeneo ambayo utafiti ulifanyika wanaona kuwa mtoto mwenye ulemavu hana thamani, ni laana na adhabu waliyopewa na Mungu kwa familia kupata mtoto huyo. Aidha, washiriki wengine walikuwa na maoni kwamba watoto wenye ulemavu huenda shule ili kucheza tu na wenzao. Wanaweza kujifunza kwa kiasi kidogo sana ikilinganishwa na wenzao wasio na ulemavu. Hivyo, kwa mujibu wa wahojiwa hao, kumpeleka mtoto mwenye ulemavu shuleni ni kupoteza pesa, rasilimali na muda. Matokeo yake, baadhi ya wazazi waliripotiwa kuficha watoto wao, hasa wale wenye ulemavu mkubwa wa akili na uziwi, na waliamua kutowapeleka shule kwani kufanya hivyo kungeleta aibu na fedheha kwasababu watafanya vibaya kwenye masomo.

Mwalimu mmoja wa darasa la awali alikuwa na haya ya kusema: *"Wazazi wanasita kupeleka watoto wao wenye ulemavu shuleni kwasababu wanahisi ni kujidhalilisha. Wengi wao, kama sio wote, wanafikiria kwamba njia bora ni kuwaficha ndani watoto wao na hakuna kufanya chochote na kutowaruhusu kuchangamana na watu wengine nje".*

Sambamba na hilo "Afisa Elimu maalum," wa wilaya mojawapo alisema:

> *"Kikwazo kikubwa ni tabia ya jamii ya kuficha watoto wenye ulemavu kwasababu wanaona aibu kuwaleta shuleni. Kwa hivyo, tunaweza kuwa na watoto walemavu katika darasa jumuishi lakini hiyo inaweza isionyeshe kutupa idadi yao halisi katika wilaya. Mara nyingi, tunatumia viongozi wa vijiji, waalimu na maafisa elimu kata kuwabaini na kuwasajili watoto kama hawa kwenye mfumo wa elimu-jumuishi. Hadi sasa, tuna wanafunzi 258 wenye ulemavu katika mfumo wa elimu jumuishi katika wilaya yetu."*

### 3.5.2 Matakwa ya wazazi kuwaandikisha watoto wao kwenye wenye ulemavu shule maalum badala ya shule jumuishi

Wakati wa majadiliano ya kikundi, washiriki wengine walitoa maoni kwamba watoto wote bila kujali ulemavu wao wako sawa. Kwa mujibu wa washiriki, mtoto aliye na ulemavu kama mtoto mwingine yeyote anastahili haki ya elimu na hivyo wanapaswa kupata fursa sawa ya elimu. Washiriki walitoa maoni kwamba ikiwa watoto wenye aina tofauti za ulemavu kama vile ulemavu wa akili na kuona, na ulemavu mwingine, wakipewa msaada wote muhimu ikiwa ni pamoja na kufundishwa mmoja mmoja, na kuzingatia mahitaji maalum ya rasilimali za kujifunzia kama vile mashine za Breli, maandishi makubwa, vitimwendo, na vifaa maalum vya kuongeza usikivu, wakalimani wa lugha ya ishara na kadhalika, wangeweza kujifunza kwa kasi sawa na watoto wa kawaida. Hata hivyo, washiriki walisema kuwa zana hizi zilikuwa hazipatikani katika shule za kawaida. Matokeo yake, wazazi waliamua kuwabakiza watoto wao wenye ulemavu nyumbani kwa sababu walitarajia kuwa watoto wao hawataweza kunufaika na mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Mzazi mmoja wakati wa majadiliano katika vikundi mjadala alisema:

> *"Kusema kweli, katika eneo letu, wazazi wako tayari sana kuwapatia watoto wao elimu bila kujali ulemavu wao. Watoto wote ni sawa na wanachukuliwa kwa usawa na kupata mahitaji ya msingi kama chakula, nguo na malazi kutoka kwa wazazi, isipokuwa tu, wanakabiliwa na changamoto katika mfumo rasmi wa elimu. Kwa mfano, mtoto aliye na shida ya kusikia anapaswa kufundishwa kwa msaada wa mkalimani wa lugha ya ishara, ambaye ni nadra kupatikana katika shule zetu na hivyo wazazi huchagua kutompeleka mtoto shuleni. Serikali inapaswa kuajiri wakalimani wa lugha ya ishara ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu".*

Maoni kama hayo yalitolewa na washiriki wengine wakiwemo maafisa katika ngazi za mikoa na wilaya, wakuu wa shule na walimu wa madarasa ya awali. Kwa mfano, 53% ya wakuu wa shule zilizotembelewa walieleza kuwa, watoto wenye ulemavu wa umri wa kuandikishwa elimu ya awali wanapaswa kusoma shule maalum na siyo shule za kawaida.

Tunajifunza kutokana na takwimu hizi kwamba kulikuwa na dhana na imani potofu miongoni mwa washiriki juu ya watoto wenye ulemavu na elimu yao. Licha ya kutambuliwa kuwa watoto wote wanastahili kupata elimu, wanajamii wengine walihisi kuwa watoto wenye ulemavu walionekana kama mzigo na fedheha kubwa kwa familia, na jamii kwa ujumla. Wanajamii wengine waliamini kuwa watoto wenye ulemavu hawawezi kuandikishwa katika mfumo wa elimu jumuishi, badala yake wanapaswa kupelekwa katika shule maalum. Kutokana na maoni ya washiriki, madarasa ya awali hayana zana zinazokidhi mahitaji ya kufundishia watoto wenye ulemavu, kama vile ulemavu mkubwa wa akili na kusikia. Kwahiyo, wazazi wangependelea kuwaandikisha watoto wao kwenye shule maalum. Kutokuwepo kwa shule maalum ndani ya jamii, watoto hao waliishia kuachwa nyumbani. Pamoja na hayo, wazazi wengine waliamini kuwa baadhi ya watotoe wenye ulemavu hawawezi 'kufundishika', wazito kuelewa na wagonjwa.Kwahiyo, hawakuandikishwa shule za kawaida. Hivyo, ilikuwa ni kupoteza muda kusajili watoto kama hawa shuleni.

### 3.5.3 Umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shuleni

Takribani 57% ya wakuu wa shule katika shule zilizotembelewa waliripoti kwamba idadi kubwa ya wanafunzi wa madarasa ya awali ikiwa wakiwemo wenye ulemavu hutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shule. Wakati wa mahojiano na majadiliano ya vikundi, ilibainishwa wazi kuwa wanafunzi wengine wenye ulemavu na wasio na ulemavu walikuwa wakitembea kwa muda wa dakika 28 kwenda na kurudi kutoka shuleni. Wakati wengine wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 12 kila siku. Umbali mrefu ulikuwa ni changamoto kwa wazazi kwa sababu wanapata shida kuwapeleka watoto wao shuleni kila siku na wakati huohuo waweze kutekeleza kazi zao za shamba, ambazo zilionekana kuwa ndio chanzo cha mapato kwa familia.

Kwa mujibu wa washiriki, baadhi ya watoto wenye ulemavu wakati mwingine walihitaji kupanda pikipiki kwenda shuleni, kwasababu hawakuweza kutembea peke yao. Hii ilikuwa miongoni mwa mambo yaliyolalamikiwa na wazazi; gharama za kila siku za usafiri zilikuwa kikwazo kwao. Kwa hivyo, umbali mrefu uliwazuia watoto wenye ulemavu kufika shuleni, kama ilivyosemwa na mmoja wa wazazi:

> *"… Ni changamoto kwa wazazi na watoto wenye ulemavu. Inawezekanaje kwa mtoto mwenye ulemavu wa akili kutembea umbali wa hadi kilomita sita peke yake kwenda shule? Wazazi wangeweza kushughulikia suala hilo, lakini wanawezaje kufanya hivyo, wakati wanahitaji pia kufanya kazi katika mashamba yao ili waweze kuhudumia familia."*

## 3.6 Utayari wa shule na madarasa kukidhi mahitaji ya utoaji elimu ya awali jumuishi

Utafiti huu ulitaka kuelewa kwa jinsi gani shule na vyumba vya madarasa viliandaliwa ili kukidhi mahitaji na kuwezesha ushiriki wa watoto wenye ulemavu wa kuyafikia na kushiriki katika madarasa jumuishi ya elimu ya awali. Utayari wa shule na vyumba vya madarasa kwa elimu-jumuishi ulipimwa kwa kuangalia miundombinu, rasilimali na vifaa vya kufundishia-kujifunzia, mchakato wa ufundishaji na upatikanaji wa walimu wenye mafunzo pamoja na mitazamo yao kuhusu elimu-jumuishi.




Kielelezo cha 10: Utayari wa shule na madarasa kutoa elimu ya awali jumuishi

### 3.6.1 Utayari wa shule na walimu wa awali kuwahudumia watoto wenye ulemavu katika mazingira jumuishi.

Utafiti ulitaka kuelewa utayari wa wakuu wa shule na walimu kushughulikia wanafunzi wenye ulemavu katika mazingira ya elimu ya awali jumuishi shuleni. Utayari, katika muktadha wa utafiti huu, unamaanisha mafunzo kuhusu elimu jumuishi. Ilibainika kuwa ni wakuu wa shule 42.2% tu ndio wamewahi kuhudhuria kozi ya kufundisha watoto wenye ulemavu, kati yao, 42.9% walihudhuria kozi ambayo iliendeshwa kwa kipindi chini ya mwezi mmoja, wakati 8.9% tu ndio waliohudhuria kozi ya mwaka mmoja. Karibu 37.1% walihudhuria kozi ya siku chache tu. Hata hivyo, wakuu wa shule 25.3% tu, wamehudhuria kozi ya elimu-jumuishi katika kipindi cha miezi kumi na mbili iliyopita.

Kama ilivyoelezwa sehemu nyingine, jumla ya walimu 77 wa madarasa ya awali walishiriki kwenye utafiti huu. Waalimu wengi (70%) walikuwa na elimu ya Astashahda ya Ualimu Daraja la III A, wakati 22% walikuwa na Stashahada ya Elimu. Walimu 74% waliripoti kuwa wamepata mafunzo kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya ya awali ya mtoto (ECD). Utafiti huo uligundua zaidi kuwa ni 24% tu ya walimu ndio waliopitia mafunzo ya elimu maalum wakati 15% waliripoti wamewahi kuhudhuria mafunzo ya kazini kuhusu elimu jumuishi ndani ya miezi 12 iliyopita.




Kielelezo cha 11: Asilimia ya Wakuu wa shule wanaokubali au kukataa kauli kwamba; 'watoto wenye ulemavu wa elimu ya awali wanaongeza mzigo kwa walimu.

**Chanzo: Data za utafiti**

Uchambuzi huo unaonesha zaidi ya nusu ya waalimu wa shule za umma walihisi hawana mafunzo ya kutosha kutoa huduma mbalimbali za kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu kwenye darasa jumuishi la awali. Ilibainika pia kuwa 68% ya walimu wa shule za Serikali walisema kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu kwenye madarasa jumuishi kuliongeza mzigo wa kazi yao. Maoni kama hayo yalitolewa na wakuu wa shule (Angalia **Kielelezo cha 11**). Karibu 59% ya walimu waliohojiwa walikubaliana na Kauli kwamba, kuwajumuisha wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu kwenye darasa la kawaida kulisababisha changamoto wakati wa mchakato wa kufundisha na kujifunza.

## 3.6.2 Mazingira ya Shule

### 3.6.2.1 Kupitika kwa njia na majengo ya shule

Uchambuzi wa data unaonesha kuwa shule nyingi zilizotembelewa hazijaandaliwa vizuri kusaidia upitaji na ushiriki wa watoto wenye ulemavu kwenye elimu ya awali. Kwa mfano, karibu 66% ya shule tulizotembelea zina ngazi, kokoto, mawe na sakafu iliyochakaa. Utafiti uligundua zaidi kuwa ni shule 16% tu zilikuwa na njia maalum za kupita watu wenye ulemavu, ambazo zilikuwa katika hali nzuri, shule 35% hazina njia hizo kabisa, wakati shule 35% zilikuwa na njia za walemavu na sakafu nzuri kwenye baadhi ya maeneo maalum, hasa kwenye vyumba vya madarasa maalum kwa watoto wenye ulemavu. Hii inaonesha kuwa watoto wenye ulemavu wanaweza kupita kiurahisi baadhi ya maeneo.



Picha kutoka eneo la utafiti: Inaonesha ngazi yenye njia ya walemavu (kushoto) na ngazi isiyo na njia ya kupita wenye ulemavu (kulia)

### 3.6.2.2 Kupitika kwa vyoo

Shule nyingi zina vyoo vya shimo, ingawa viko katika hali tofauti. Vyoo vingine vilikuwa katika hali nzuri wakati vingine havikuwa na hali nzuri. Karibu 75% ya shule zote hazina vyoo vilivyorekebishwa kwa ajili ya watoto wenye ulemavu. Kwenye shule hizi, watoto wenye ulemavu walikuwa wanachangia vyoo na watoto wengine. Ni shule 15% tu ndizo zimerekebisha vyoo ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu. Karibu 10% ya shule zina vyoo vya watoto wenye ulemavu; Hata hivyo, havijarekebishwa ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu. Havikuwa na njia za walemavu na siyo visafi. Shule nyingine zilibainika kuwa na vyoo lakini havikuwa vikitumika. Kwa mfano, katika moja ya shule za msingi zilizotembelewa Manispaa ya Tanga, kulikuwa na vyoo maalum vilivyotengwa kwa ajili ya watoto wenye ulemavu, lakini vilikuwa havitumiki, badala yake, vilitumika kama stoo ya chupa tupu za maji. Vile vile, katika shule nyingine, vyoo vya watoto wenye ulemavu vilikuwepo na viko katika hali nzuri, lakini havikutumika kwani kila siku vilikuwa vimefungwa. Pia ilibainika kuwa 70% ya shule zilizotembelewa hazikuwa na vyoo vilivyotengwa kwa wanafunzi wa awali. Hivyo, wanafunzi wa delimu ya awali walichangia vyoo na wanafunzi wa madarasa mengine.

## 3.7 Mpangilio wa darasa na hali ya hewa

Kimsingi, darasa jumuishi la awali ni lile ambalo uwiano kati ya mwalimu na wanafunzi unaendana na miongozo iliyowekwa (1:25 au chini). Mwalimu wanapewa mafunzo ya kitaalam kufundisha wanafunzi wa darasa la awali ikiwa watoto wenye ulemavu mbalimbali na wanatakiwa kuwa na msaidizi wa kuhakikisha wanafunzi wote wanahudumiwa. Darasa linatakiwa lipitike kwa wanafunzi wote na liwe "darasa linaloongea" lililosheheni zana na vifaa vya kujifunzia na kufundishia vinavyowavutiwa watoto.

### 3.7.1 Kukosekana kwa darasa lililojengwa maalum kwa ajili ya elimu ya awali

Utafiti huo uligundua kuwa 72.5% ya shule zina darasa lililotengwa maalum kwa wanafunzi wa darasa la awali. Hata hivyo, kati ya madarasa yaliyotengwa 66% yalikuwa yamepangwa kama madarasa ya shule ya msingi bila kuwa kona za kujifunzia, madawati yalipangwa kwa safu, na hakuna machapisho ya kubandikwa darasani. Ni 32% tu ya vyumba vya madarasa vinaweza kuelezewa kuwa vinafaa, vina madawati yanayoendana na watoto, kona za kujifunzia, na machapisho ya kubandika darasani. Kwenye shule nyingine (karibu 7.5%) ya watoto wa darasa la awali walikuwa wanachangia vyumba vya madarasa na watoto wengine. Karibu 3.8% ya shule zilizotembelewa, wanafunzi wa darasa la awali hawakuwa na darasa maalum la awali au darasa la kuchangia na madarasa mengine. Madarasa yao yalikuwa yanaendeshewa nje mahali pa wazi.



Picha ilipiwa eneo la utafiti ikionyesha mpangilio wa darasa la awali unaofanana na madarasa ya shule za msingi. Madarasa ya awali ya msingi yanapaswa kuwa na kona za kujifunzia, machapisho mengi ukutani mpangilio wa kukaa kwa duara.




Kielelezo cha 12: Matokeo kutoka maeneo ya utafiti juu ya hali ya mpangilio wa madarasa ya awali na urahisi wake

**Chanzo: Taarifa za utafiti**

Kielelezo cha 12 kinaonesha, 37% ya madarasa yaliyotembelewa yana nafasi za wazi kati ya dawati na dawati, yamepangwa kwa safu, na kuwapa wanafunzi urahisi wa kutembea. Pia inaonesha kuwa ni 13% tu ya madarasa yaliyochunguzwa wanafunzi wenye mahitaji maalum walikuwa wameketi madawati ya mbele.

Kati ya madarasa yaliyochunguzwa, 53% yalikuwa na madawati ya kutosha watoto wote. Madawati yaliyokaguliwa darasani yanafaa kwa watoto wadogo. Ni 14% tu ya madarasa ambayo wanafunzi walikuwa wameketi kwenye mikeka, sakafuni. Madarasa haya yanaweza kuelezewa kuwa ndiyo yako sahihi kwa wanafunzi wa darasa la awali kwani wamefuata mwongozo wa mtaala. Kwenye madarasa mengi yaliyotembelewa, watoto walikuwa wameketi wakimtazama mwalimu mbele ya darasa.

Karibu ufundishaji wote uliokaguliwa ulikuwa wa kawaida unahusisha darasa zima, ukitumia mbinu zile zile zilizooeleka na ulilenga katika kumaliza silabasi bila kujali mahitaji ya kujifunza ya wanafunzi. Hakukuwa na ushahidi kwamba walimu walirekebisha mtaala ili ukidhi mahitaji tofuati ya kujifunza na matokeo ya kufundisha na kujifunza.

### 3.7.2 Upungufu wa Vifaa vya kujifunzia na kufundishia

Darasa jumuishi linahitaji kila mtoto awe na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kusaidia shughuli zao za kufundisha na kujifunza. Utafiti uligundua kuwa kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia-kujifunzia. Karibu walimu wote(80%) waliohojiwa wa shule za awali walikuwa na mtaala wa awali, silabasi na kiongozi cha walimu. Lakini, karibu shule zote zilizotembelewa mikoa yote, vitabu vya kiada vilivyorekebsihwa, hasa kwa watoto wenye uoni hafifu, havikuwepo. Hii inaweza kuwa kikwazo kubwa kwenye kufikia lengo la elimu-jumuishi ambalo linahitaji kila mtoto apate elimu bila kujali ulemavu wake. Mmoja wa maafisa wa elimu wa wilaya alikuwa na haya ya kusema

> *"… Hivi karibuni nilipokea vitabu vichache vya vya maandishi ya nukta nundu(Braille), na mtaala hautoshelezi mahitaji. Tuna viku maandishi vichache sana, mashine za Braille na karatasi za Braille chache pia. Kwa mfano, watoto watano wanalazimika kuchangia mashine moja ya Braille. Hivyo, ni ngumu sana kufikia matokeo yaliyolengwa bila kuwa na rasilimali za kusaidia."*

Mtaala wa elimu ya awali unahimiza kuwepo vifaa mbalimbali katika muundo kuchezea, kuigiza, sanaa, vitabu vya hadithi zinazovutia ili viwasaidie watoto kwenye ujifunzaji na kucheza. Hata hivyo, kama Kielelezo cha 13 kinavyoonesha shule zina vifaa vichache vya kufundishia-kujifunzia. Uchambuzi wa data unaonesha zaidi ya walimu 70% wa madarasa ya awali hawakuwa na vifaa stahiki vya kufundishia na kujifunzia watoto wenye ulemavu. Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia hupunguza fursa za watoto kuchangamana na kushirikiana kujifunza wakiwemo wenzao wenye ulemavu.




Kielelezo Na: 13: Hali ya uwepo wa vifaa vya kufundisha na kujifunzia kwa Watoto awali wenye Uremavu.

## 3.8. Ufundishaji na Ujifunzaji

Ingawa wakuu wa shule 74% waliripoti kuwa walimu wa awali ni wepesi kupokea mabadiliko na kurekebisha mtaala na shughuli za ujifunzaji ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu, uchunguzi wa darasani unaonesha kuwa hakuna ushahidi walimu walitumia mikakati tofauti ya kufundisha ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanajifunza na wanaweza kushiriki kwa ufanisi. Iliripotiwa kuwa baadhi ya walimu hawakuwa tayari kurekebisha ufundishaji, kama ilivyoelezwa na Afisa Elimu Wilaya mmoja;

> *"... Walimu wa shule za awali ni walimu wa kawaida, ambao kwa kawaida huchaguliwa/kuteuliwa kufundisha madarasa ya awali. Hawana ujuzi wa kutosha kushughulika na kuendeleza Maudhui, wala kurekebisha ufundishaji ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu. Kwa maoni yangu, muda mwingi, watoto wenye ulemavu wananyimwa fursa ya kushiriki vyema kwenye ujifunzaji."*

Mikakati inayoripotiwa kutumika zaidi kuwasaidia watoto wenye ulemavu ni pamoja na kuwaweka viti vya mbele darasani, na kuwapatia muda wa ziada kujifunza na kufanya kazi za masomo. Mkakati mwingine ulioripotiwa ni pamoja na kurudia darasa ili kuwasaidia watoto ambao hawakufikia malengo ya kujifunza. Ushahidi ulikosekana kuthibitisha kama walimu huandaa somo lenye maelekezo ya kipekee na kutofautisha malengo ya kufundisha, ili kukidhi mahitaji ya kujifunza kwa wanafunzi tofauti. Kukosekana kwa maelekezo ya kipekee kwenye ufundishaji kunaweza kuhusishwa na uwiano mkubwa wa mwalimu kwa mwanafunzi, mzigo mkubwa kwa walimu na ufinyu wa muda.




Kielelezo cha 14. Asilimia ya walimu waliokaguliwa wakitumia mbinu mbalimbali za kufundishia

**Chanzo: Takwimu za Utafiti**

Kielelezo 14 kinaonesha asilimia ya uchunguzi wa jinsi waalimu wanavyotumia mbinu tofauti za kufundishia kukidhi mahitaji ya kujifunza ya wanafunzi wote. Hata hivyo, kwenye madarasa mengi, mwingiliano wa mwalimu na mwanafunzi ulikuwa mzuri. Hakukuwa na ishara kwamba walimu waliwatenga wanafunzi wenye ulemavu kushiriki kwenye somo. Walimu walionekana kuwajali na kuwapenda wanafunzi wote. Masimulizi yafuatayo kutoka kwenye moja ya madarasa yaliyoonesha mwingiliano wa mwalimu na mtoto mwenye ulemavu kwenye mazingira jumuishi

*"… Wakati wa uchunguzi kwenye darasani moja, mwalimu wa shule ya awali aliwaambia wanafunzi wahesabu kwa sauti kuanzia 1hadi 10. Wanafunzi kadhaa walijitolea akiwemo mwanafunzi mmoja ambaye baadaye mwalimu wake alimuelezea kuwa alikuwa na ulemavu wa akili (II). Kwa bashasha , alihesabu kikamilifu kuanzia 1hadi 10. Kisha mwalimu aliwaambia wanafunzi kujitolea kuandika 1hadi 10 kwenye ubao. Wanafunzi watatu walifanya hivyo kwa usahihi kabisa. Kwa mara nyingine, mwanafunzi huyo alijitolea. Hata hivyo, mara hii wanafunzi wenzake walipiga kelele, "Hawezi kufanya hiyo". Mwanafunzi huyo hakurudi nyuma na mwishowe mwalimu alimchagua. Alipokwenda ubaoni , aliandika zero kadhaa mfululizo na akaondoka akiwa na hisia ya kufanikiwa. Mwalimu alimpongeza na darasa lote likampigia makofi.*

## 3.9 Sababu nyingine zinazozuia elimu jumuishi

### 3.9.1 Kukosekana kwa mbinu makini za kutambua watoto wenye ulemavu wakati wa kujiunga shule ya awali

Kama ilivyoelezwa huko nyuma, moja ya malengo ya elimu ya awali ni kutambua watoto wenye mahitaji maalum na kutoa afua stahiki wakati wanajiunga elimu ya awali. Ili kutambua utaratibu au tathmini ya utaratibu inahitaji zana ya kuchunguzia. Utafiti huu ulitaka kujua kama kulikuwa na mbinu yoyote au zana za upimaji kusaidia shule na waalimu kutambua watoto wenye mahitaji maalum ya elimu.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa hakuna zana za kuchunguzia/kupimia zilizowekwa kwa ajili ya utambuzi wa watoto wenye mahitaji maalum wakati wa kuingia shule ya awali. Shule/walimu walitegemea sana uchunguzi wa kila siku wa mwalimu wakati wa mchakato wa kufundisha na kujifunza (88%) na njia nyingine kama ripoti ya wazazi na mahojiano ya ana kwa ana na mtoto. Hii inaonesha kuwa utambuzi wa mapema wa watoto siyo jambo la kudumu ni la dharura pale inapohitajika. Ingawa njia hizi haziwezi kupuuzwa, taratibu hizi zimesaidia kuelimisha, lakini bado kuna hitaji la kuwa na zana ya kitaifa ya kufanyia utambuzi wa mapema.

### 3.9.2 Kukosekana kwa mafunzo kazini kwa walimu wa awali

Walimu wengi hawana mafunzo ya kuwajengea uwezo unaohitajika kusimamia madarasa jumuishi, matokeo yake wanakwepa kufundisha madarasa hayo. Kushughulikia darasa jumuishi kunaongeza mzigo wa kazi kwa mwalimu lakini mzigo unakuwa mzito zaidi kwa kukosekana kwa ujuzi muhimu wa kushughulikia darasa jumuishi. Hii imeelezwa vizuri na mwalimu mmoja wa shule ya awali:

> *"… Hebu fikiria, kuwa na watoto wa kawaida na walemavu kwenye darasa moja kunaongeza mzigo kwa mwalimu. Inakuwaje pale mwalimu kama huyo hajui kusimamia madarasa kama haya? Jibu ni dhahiri, kwamba, mzigo kwa mwalimu unazidi kuwa mgumu. "*

Vile vile, Afisa elimu maalum alisema haya:

> *"Tuna uhaba mkubwa wa walimu wa elimu maalum. Kwa mfano, kuna waalimu watano tu wa wanafunzi wenye mahitaji maalum ya elimu ndani ya vituo sita vya elimu maalum katika wilaya yetu, baadhi yao hawana ujuzi wa kushughulikia zaidi ya ulemavu mmoja. Mwalimu aliyefundishwa kushughulikia wanafunzi viziwi hana ujuzi wa kuwahudumia wanafunzi wenye ulemavu wa akili. "*

### 3.9.3 Upungufu wa Wafanyakazi wenye mafunzo ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu shuleni

Waalimu wengi waliohojiwa walisema kwamba hawajawahi kupata mafunzo yoyote yaliyotolewa kusaidia watoto wenye ulemavu kwenye madarasa jumuishi. Hivyo, wengi wao wanatumia uzoefu wao kuwasaidia watoto kama hao, na matokeo yake shule zinakataa kwa njia isiyo rasmi kuwapokea watoto wenye ulemavu. Walimu wa shule za awali walikuwa na maoni kwamba wanahitaji ujuzi kama vile kuwatambua mapema, kugundua na kutoa msaada wa mapema kwa watoto wenye ulemavu. Changamoto kubwa ni kwamba wakati fulani, watoto wenye ulemavu wanaweza kuwapo darasani lakini walimu hawana uwezo wa kutambua, kugundua na kutoa msaada wa mapema unaohitajika kwa watoto kama hao wakati wa mchakato wa kufundisha na kujifunza. Hii ilielezwa na mmoja wa walimu wa shule ya awali, alisema:

> *"… Nilikuwa nikifanya kazi kama mwalimu wa shule ya msingi wa darasa la kwanza na la tatu. Baadaye nikahamishiwa darasa la awali jumuishi. Ilikuwa ngumu sana kwangu kwani sikupewa aina yoyote ya mafunzo ya jinsi ya kufundisha darasa jumuishi la awali. Sikujua nifanye nini kutambua, kugundua na kutoa msaada unaohitajika kwa watoto wa shule ya awali ambao walikuwa na aina tofauti za ulemavu kama vile ualbino, ulemavu wa akili na viungo. " Hii ilifanya kazi yangu kuwa ngumu zaidi. "*

### 3.9.4 Ufadhili mdogo/uhaba wa fedha

Utafiti ulitaka kujua ufadhili wa fedha kwa ajili ya watoto wa shule ya awali wenye ulemavu. Mahojiano na maafisa wa wizara za (MoEST na OR-TAMISEMI) yanaonesha kuwa hakukuwa na ufadhili maalum kwa watoto wa shule ya awali wenye ulemavu. Kwa kuwa elimu ya shule ya awali ni sehemu ya elimumsingi, kwahiyo inafadhiliwa kupitia ruzuku, ambayo Tsh 10,000 kwa kila mwanafunzi. Kuhusu matumizi ya kiasi kinachotengwa, 60% inatarajiwa kwenda moja kwa moja shuleni wakati asilimia 40 iliyobaki hutumiwa kununua vitabu vya kiada. Hata hivyo, matokeo kutoka kwa wakuu wa shule, yanaeleza kuwa ruzuku ya wanafunzi inayopokelewa haikujumuisha watoto wa shule ya awali. Kwa kuongezea, ruzuku ya wanafunzi haitolewi kwa usawa. Hivyo, hakuna fungu au ufadhili maalum kutoka serikalini kwa ajili ya wanafunzi wa shule za awali.

Wakuu wa shule waliulizwa zaidi kama kuna fedha za kusaidia wanafunzi wa shule za awali wenye ulemavu katika mazingira ya elimu jumuishi. Karibu 72.3% ya shule zilizotembelewa wakuu wa shule walikiri kwamba hakuna fedha za ziada kusaidia wanafunzi wenye ulemavu. Wakuu wachache wa shule waliripotiwa kuwa na fedha za ziada, ambazo walizipata kutoka vyanzo mbalimbali kama michango ya wazazi (30.4%), fedha kutoka kwa wafadhili (56.5%), miradi ya kujitegemea shuleni (39.1%) na vyanzo vingine (34.8%).

Uchambuzi wa mapendekezo ya kurekebisha fomula ya kugawa Ruzuku ya Wanafunzi (2017) yanaonesha kuwa rasimu ya fomula imezingatia haki. Inazingatia seti ya vipengele/vigezo vingi zaidi ya idadi ya wanafunzi, inaangalia pia uwepo wa wanafunzi wenye mahitaji maalum shuleni. Fomula inashughulikia mahitaji mapana na masuala ya haki na usawa. Kwa mujibu wa afisa huyo wa wizara, fomula hiyo bado haijapitishwa rasmi kwa utekelezaji.

## 3.10 Tofauti ya miundombinu ya Shule kwa makundi ya shule

Utafiti ulihusisha makundi matatu ya shule ambazo ni shule mchanganyiko, shule jumuishi na shule za kawaida. Malengo ya kuhusisha makundi haya matatu ya shule ilikuwa kufahamu kama kuna tofauti ya upatikanaji wa miundombinu ya kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu wa shule za awali. Matokeo yanaonesha kuwa shule jumuishi za serikali hazina miundombinu ya kutosha ikilinganishwa na shule mchanganyiko. Kwa mfano, asilimia 75 ya shule jumuishi hazina vyoo vilivyotengwa maalum kwa wanafunzi wenye ulemavu. Wanafunzi wenye ulemavu wanachangia vyoo na watoto wengine. Asilimia 57 ya shule mchanganyiko (Shule yenye vitengo vya elimu maalumu pamoja na jumuishi) hazina vyoo kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu. Karibu 34% ya shule jumuishi hazina njia za walemavu ikilinganishwa na asilimia 30 ya shule mchanganyiko.

## 3.11 Hatua na Vitendo vyenye Mafanikio

### 3.11.1 Bango la kuhamasisha jamii juu ya haki ya elimu kwa watoto wenye ulemavu

Ili kubadilisha mitazamo na mawazo potofu juu ya watoto wenye ulemavu, moja ya shule mchanganyiko iliyotembelewa ilibuni bango, ambalo lilitetea haki za watoto kupata elimu, kupendwa, kuthaminiwa, kutonyanyapaliwa na kutobaguliwa




Picha ya utafiti: ikionesha bango la kuhamasisha jamii juu ya haki ya elimu kwa watoto wenye ulemavu

### 3.11.2 Kuwepo kwa Njia za wenye Ulemavu

Kwa madhumuni ya kutokujulikana, shule hizi mbili zilizotajwa sehemu ifuatayo zinaitwa shule "Y" na shule "X". Majengo yote ya shule ya 'Y' yana njia za wenye ulemavu, na hivyo majengo yote wanapitika na kufikika kiurahisi na watoto wenye ulemavu wa viungo, hasa wale wanaotumia kitimwendo.



**Picha ya utafiti ikionesha njia za wenye ulemavu kwenye mlango wa kuingilia darasani shule 'Y'.**

### 3.11.3 Vyoo vilivyorekebishwa

Shule 'X' ni shule ya msingi ya umma iliyoko mkoa mmojawapo ulioshiriki kwenye utafiti. Shule hiyo imeteuliwa kuwa moja ya shule jumuishi. Inaandikisha watoto wenye ulemavu wa viungo. Shule ina vyumba 8 vya madarasa kimoja kwa ajili ya watoto wa darasa la awali. Licha ya ukweli kwamba shule hiyo haina vyoo maalum kwa watoto wa shule ya awali,  ina vyoo viwili vya kusukuma maji vilivyorekebishwa kwa ajili ya watoto wenye ulemavu. Hata hivyo, kwa mujibu wa mhojiwa, maji hayapatikani mara kwa mara. Vivyo hivyo, kwenye shule 'Y' ambayo pia in choo kilichorekebishwa.



**Choo kilichorekebishwa Shule 'X'**

### 3.11.4 Upatikanaji wa Vifaa vya Kuchezea nje

Pia ilibainika kuwa shule ya 'Y' ilikuwa na vyumba viwili vya madarasa vilivyowekwa kwa ajili ya watoto wa darasa la awali na vifaa vya michezo ya nje kama vile bembea, kwa ajili ya watoto wa shule ya awali. Mbali na hayo, shule ina pampu ya maji kwa ajili ya kujaza maji kwenye matanki makubwa mawili. Hivyo, shule ina maji ya bomba yanayotumika kunywa, bustani na huduma nyingine.

### 3.11.5 Mambo yaliyochangia Utendaji wenye Mafanikio

Utafiti ulitaka kufahamu mambo yaliyochangia kuleta hatua zenye mafanikio. Matokeo yanaonesha licha ya ukweli kwamba uongozi wa shule ulikuwa muhimu kuchagiza mafanikio, kulikuwa na mchango wa wadau wengine wa nje ya shule kama mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za kidini. Kwa mfano, vyoo vya shule 'X' vilivyorekebishwa walipata msaada kutoka kituo cha watoto wenye walemavu cha kidini kilicho karibu na shule. Kituo hicho kinalea watoto wenye ulemavu, ambao huandikishwa shuleni 'X'. Kituo hicho kiliipatia shule misaada ya vifaa na ukarabati wa shule. Vivyo hivyo, pampu ya maji na vyoo vilivyorekebishwa kwenye shule 'Y' vilisaidiwa na shirika lisilo la kiserikali. Kwahiyo, kutokana na haya tunajifunza na kugundua kuwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni moja sababu zinachangia mafanikio kwenye jamii.



**Picha ya utafiti-ikionesha vifaa vya michezo ya nje ya darasa kwenye shule 'Y'.**

# 4. Hitimisho na Mapendekezo

## 4.1. Hitimisho

Serikali ya Tanzania imeonesha nia na jitihada za kupongezwa kwenye kuwezesha upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu kupitia sera, sheria na mikakati yake. Sera, sheria na miongozo siyo tu inaelekeza wazi kabisa haki ya elimu kwa watoto wote, bali pia inatoa maagizo rasmi kwamba shule zote zinapaswa kuwa jumuishi na zikidhi mahitaji ya wanafunzi wote.

Hata hivyo, utafiti umeonesha kuwa dhamira ya kisera siyo lazima kuwa halisia. Shule na madarasa mengi bado havijaandaliwa vya kutosha kuwahudumia wanafunzi wa shule za awali wenye ulemavu. Upatikanaji na ushiriki mzuri wa wanafunzi wa shule ya awali wenye ulemavu kwenye mazingira ya elimu jumuishi unatishiwa na baadhi ya vikwazo vya kiuchumi na kijamii, ikiwemo unyanyapaa dhidi ya watoto wenye ulemavu na familia zao, mitazamo hasi ya wanajamii na wazazi juu ya kusomesha watoto wenye ulemavu, na baadhi ya waazi wanawaficha ndani watoto wao wenye ulemavu.

Changamoto nyingine ni pamoja na ufadhili mdogo/uhaba wa fedha za kugharamia huduma na mahitaji ya watoto wenye ulemavu, idadi ndogo ya walimu, waliopata mafunzo kuhusu elimu maalum na elimu-jumuishi, kukosekana kwa miundombinu iliyorekebishwa, vyumba vya madarasa maalum, ufundishaji rafiki kwa wenye ulemavu na vifaa vya rafiki vya kufundishia na kujifunzia (Braille). Pia, mtaala sio rahisi kubadilika. Hakuna vigezo maalum vya madarasa jumuishi, wala mbinu za kimfumo za kugundua na kutambua watoto wenye mahitaji maalum wakati wanajiunga na shule ya awali. Aidha, hakuna takwimu kamili za idadi ya watoto wenye ulemavu walio shuleni na ambao hawasomi shule. Hii inaleta changamoto kubwa kwenye upangaji na utoaji wa elimu bora jumuishi.

Kwa hili, utafiti huu unasema kuwa serikali ya Tanzania kupitia sheria na sera zake imedhamiria  kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu katika mazingira jumuishi. Watoto wenye ulemavu  wenye umri kuandikishwa shule ya awali wana fursa finyu ya kuingia shule. Wakibahatika kuandikishwa shule, ushiriki wao kwenye mchakato wa kufundisha na kujifunza ni mdogo. Walimu walikuwa na uwezo mdogo wa kusaidia watoto wenye ulemavu. Hii inaweza kuhusishwa na walimu kukosa mafunzo ya kuwahudumia watoto wenye ulemavu. Kwahiyo,  kuna kutofautiana kati ya dhamira na maelekezo ya sera na utekelezaji halisi shuleni.

Matokeo ya utafiti wa sasa yanasaidia matokeo ya utafiti wa huko nyuma kuhusu utoaji wa elimu jumuishi. Utafiti huo unazidi kusema kuwa licha ya kuhimiza shule jumuishi, bado shule maalum  na shule mchanganyiko zipo na zinaendelea kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu . Kwa wingi wa changamoto zinazozikabili shule jumuishi, utaratibu wa kutumia shule mchanganyiko unaweza kuwa mzuri na wenye manufaa  angalau kwa miaka michache ijayo wakati uboreshaji wa shule-jumuishi unaendelea.

## 4.2. Mapendekezo

Kulingana na matokeo, mapendekezo yamejikita kujenga uelewa, ushirikiano na ushirikishwaji wa serikali ili kuhakikisha miongozo na sera zinatekelezwa ngazi zote, ikiwemo mafunzo ya walimu. Yafuatayo yanapendekezwa:

- Kuendeleza uhamasisha wa jamii ili kukuza uelewa juu ya umuhimu wa kuwaelimisha watoto wenye ulemavu.
- Mamlaka za serikali za mitaa zitunge na kutekeleza sheria ndogo ndogo, kuwahimiza wazazi kuwaandikisha shule watoto wao wenye ulemavu badala ya kuwaficha ndani.
- kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuendeleza hatua nzuri zenye mafanikio kwenye ujumuishi na kushughulikia vikwazo vinavyozuia juhudi zinazoendelea za kutimiza mahitaji ya kielimu kwa watoto wenye ulemavu wa shule ya awali
- Kutengeneza zana rahisi itakayosaidia na kuongoza wadau wote wakiwemo walimu wa shule za awali kuwatambua watoto wenye uoni hafifu, ulemavu wa kusikia na upungufu mdogo wa kiakili wakati wa kujiunga na shule ya awali. Aina hizi za ulemavu zinaweza zisitambulike kwa urahisi kupitia kuangalia tu.
- Kutofautiana kwa utekelezaji wa elimu jumuishi shuleni kunaweza kuhusishwa na kukosekana kwa miongozo na kanuni za viwango vya darasa jumuishi na utendaji jumuishi shuleni. Kuna haja ya kuandaa miongozo na kanuni za viwango vya darasa jumuishi la awali shuleni kuwasaidia na kuwaongoza walimu kufanya vyumba vya madarasa ya watoto kuwa jumuishi zaidi.
- Kuongeza mgawo wa fedha kwenye kutekeleza na kusaidia elimu jumuishi ya awali. Njia mojawapo inaweza kuwa kuharakisha utekelezaji wa rasimu ya Fomula ya Ruzuku ya Wanafunzi, ambayo inazingatia mgawanyo wa fedha zinazotengwa maalum kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum shuleni. Ukamilishaji na kutumia fomula hii unaweza kuhamasisha matendo jumuishi.
- Kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa data zinazohusu watoto wenye ulemavu, zipange data hizo kwa umri, aina ya ulemavu na jinsia kwa ngazi zote.
- Kuboresha mitazamo ya waalimu kwa watoto wenye ulemavu na mbinu za kufundisha darasa jumuishi. Watoa mafunzo ya waalimu wanapaswa kutoa mafunzo ya walimu kazini. Kimsingi jambo hili lilitajwa na 61% ya wakuu wa shule.
- Licha ya kuwepo kwa vifungu vya kisera vya serikali vinavyohimiza kila mtoto ana haki ya kuelimishwa katika mazingira jumuishi, takwimu zinaonesha kuwa haiwezekani kwa baadhi ya mahitaji ya watoto kutimizwa wakiwa kwenye darasa la kawaida. Hii inaonesha umuhimu na hitaji la kuelimisha watoto wenye ulemavu mkubwa kwenye shule maalum au mchanganyiko ambako kuna kitengo maalum na mwalimu maalum mwenye utaalamu wa kuwasaidia kujifunza watoto wenye ulemavu.

- Licha ya vifungu vya kisera vya serikali vinavyosema kwamba kila mtoto ana haki ya kuelimishwa katika mazingira ya pamoja, data inaonyesha kwamba inaweza kuwa haiwezekani kwa mahitaji ya watoto wengine kutimizwa katika darasa la kawaida. Hii inaonyesha haja ya kuelimisha watoto wenye ulemavu mkali katika shule maalum au zilizojumuishwa ambapo kuna kitengo maalum na mwalimu maalum kusaidia ufundishaji wa watoto wenye ulemavu.

- Kuna haja kwa jamii husika kwa kushirikiana na wadau wengine kuanzisha vituo shikizi. Vituo hivi vinaweza kutoa fursa kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu ya awali kwenye shule zilizo karibu zaidi ndani ya jamii zao.
- Pitia upya mtaala na muhtasari/silabasi za elimu ya awali, uimarishe vifungu vya mitaala vinavyohusiana na viashiria vya utendaji kwa watoto wenye ulemavu wa kusikia na kuona.
- Taasisi ya Elimu Tanzania irekebishe vitabu vya kiada awali na vitabu vya hadithi vya wanafunzi wa awali ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu wa kuona (Braille).
- Chunguza matumizi ya ubunifu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya bei nafuu vinavyopatikana maeneo husika, na washirikishe wadau kutoa msaada na ushirikiano.

## Marejeo


Alisha, M. B. B. (2020). Barriers to inclusive education in Tanzania's policy environment: national policy actors perspectives, Compare: A Journal of Comparative and International Education

Corbett, J. (2001). Teaching Approaches which support Inclusive Education: A connective pedagogy. *British Journal of Special Education*, 28.

Florian, L. (2014). 'What counts as evidence of inclusive education?', *European Journal of Special Needs Education*, vol. 29, no. 3, pp. 286-294. https://doi.org/10.1080/08856257.2014.933551

Kisanga, S. E. (2017). *Educational barriers of students with sensory impairment and their coping strategies in Tanzanian Higher Education Institutions.* (PhD thesis), Nottingham Trent University.

Lehtomaki, E., M. T. Tuomi, and M. Matonya. (2014). "Educational Research from Tanzania 1998-2008 Concerning Persons with Disabilities: What Can We Learn?" *International Journal of Educational Research* 64: 32-39. doi:10.1016/j.ijer.2013.10.005.

Njjelesani, J., S. Couto, and D. Cameron. (2011). "Disability and Rehabilitation in Tanzania: A Review of the Literature." *Disability and Rehabilitation*, 33 (23-24): 2196-2207.doi: 10.3109/096638288.2011.563817

Ross-Hill, R. (2009). Teacher Attitude towards inclusion practices and special needs students. *Journal of Research in Special Education Needs, 9(3), 188-198*

Tungaraza, F. D. (2012). Including the excluded: Impediments to attaining this goal in education in Tanzania. *Specialpedagogska rapporter och notiser fran Hogskolan Kristianstad*, (Nr.9), 4-30.

The United Republic of Tanzania. (2014). Sera ya Elimu na Mafunzo. Dar es Salaam: Ministry of Education and Vocational Training

The United Republic of Tanzania. (2012 - 2016). National Basic Education Statistics in Tanzania: National Data. Ministry of Education, Science and Technology

The United Republic of Tanzania. (2017). National Basic Education Statistics in Tanzania: National Data. Ministry of Education, Science and Technology

The United Republic of Tanzania. (2018). National Basic Education Statistics in Tanzania: National Data. Ministry of Education, Science and Technology

The United Republic of Tanzania. (2019). National Basic Education Statistics in Tanzania: National Data. Ministry of Education, Science and Technology.

UNESCO. (1994). *The Salamanca statement and framework for action on special needs education.* Retrieved from http:// www.unesco.org/education/pdf/SALAMA_E.PDF

S.L B 79401, Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 (0)22 2151852/3

Nukushi: +255 (0)22 2152449

Baruapepe: info@hakielimu.or.tz

Website: www.hakielimu.or.tz